**Baba** Mtakatifu ateua maaskofu wasaidizi Dar

UKURASA 2



**Rais** auawa akiwa nyumbani kwake, mkewe mahututi

UKURASA 19




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580635

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# TUTAPUKUTIKA

## **Samia** aonya kupuuza hadhari dhidi ya corona, wizara yaanika mikakati kuikabili, TMDA yajipanga... *Endelea Uk. 2, 3 & 4*



Wananchi wakiwa katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere jana, huku wachache wakiwa wamechukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona kwa kuvaa barakoa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## BoT yaagizwa utekelezaji riba za benki




UKURASA 2



Mshindi wa gari aina ya Fortuner kwenye promosheni ya kampeni ya Bonge la Mpango ya Benki ya NMB, Abdallah Mohmed Abdalla (kulia), akikabidhiwa mfano wa funguo na Kaimu Ofisa Mkuu Ukaguzi wa Ndani wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, katika hafla iliyofanyika mkoani Morogoro. Kushoto ni Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper na Meneja Mwandamizi wa Idara ya Wateja Binafsi, Isaac Mgwasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtaalamu ataja kiini wanandoa kuuana

UKURASA 3

**MICHEZO** BENTEKE WA CRYSTAL PALACE ATUA TANZANIA UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na wananchi wa Kibaigwa, mkoani Dodoma jana, akiwa safarini kuelekea mkoani Morogoro kwa ajili ya ziara ya kikazi siku mbili. **PICHA: IKULU**

# Samia aonya 'tutapukutika' kwa corona

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania kutopuuza tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Covid-19, akionya kuwa 'watapukutika'.

Alitoa hadhari hiyo jana alipozungumza na wananchi wa Kibaigwa wilayani Kongwa mkoani Dodoma wakati msafara wake uliokuwa unatoka Dodoma kwenda Morogoro, uliposimama.

Rais Samia alisema wimbi la tatu la virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19 ni hatari zaidi kuliko yaliyopita kutokana na kuleta madhara papo hapo.

Alisema kwa kutambua hatari hiyo, kuna haja wananchi kuzingatia tahadhari zote zinazotolewa na wataalamu ikiwamo uvaaji wa barakoa.

"Nikitazama hapa ninaona waliοziba pua na mdomo ni kidogo sana. Tuchukue tahadhari zote dhidi ya corona.

"Lipo wimbi la tatu nchini, tuna wagonjwa Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Dodoma pia wapo... linapukutisha kwa wenzetu na likikufika linakupukutisha kweli," alionya.

Mbali na kutoa angalizo hilo, Rais Samia aliwaagiza viongozi wa serikali na chama kushughulikia na kutatua kero za wananchi katika maeneo yao ikiwamo suala la ardhi na kuunganishiwa umeme.

Alisema serikali itajenga kituo maalum kwa ajili ya kupozea umeme huko Kibaigwa, ili kutatua tatizo la umeme kukatika kila mara. Pia alibainisha kuwa tayari halmashauri imeanza kufanyia kazi eneo la maegesho ya magari makubwa linalohitaji Sh. milioni 80.

"Suala la umeme ninaelewa unaofika hapa ni kutoka Morogoro na hauna nguvu kubwa, inatakiwa kujengwa kituo, lakini Spika na Waziri mwenye sekta alifanyie kazi... halitachukua muda mrefu, haya mawili ninayabeba," alisema.

Rais Samia aliwataka wafanyabiashara wa eneo hilo kuzingatia na kuzifuata kanuni na sheria zilizowekwa na halmashauri ikiwamo kinamama na babalishe katika kufanya biashara zao.

"Sisi ni marafiki sana wa wafanyabiashara, tunahakikisha kila tuwezalo maisha yenu yanaenda ila mfuate kanuni.

"Pia uzingatiwe ulinzi na usalama kwenye maeneo yetu na anayeingia katika maeneo yetu tuseme.

"Nimeambiwa kuna viongozi wangu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ama wanauza au wanakodisha maeneo bila kushauriana na wananchi. Waziri atakuja kusikiliza ili kuondoa migogoro na wananchi," aliagiza.

Rais aliyataka makundi maalum, wakiwamo wenye ulemavu, kujiunga kwenye vikundi ili kunufaika na mikopo ya halmashauri.

Spika wa Bunge na Mbunge wa Kongwa, Job Ndugai, alisema jimbo hilo lina wakazi takriban 400,000, huku akibainisha kwamba tayari Kibaigwa wameanza kupokea fedha za miradi ya maendeleo zikiwamo Sh. milioni 120 zilizotolewa kwa ajili ya elimu.

Akiwa Msamvu mjini Morogoro, Rais Samia aliagiza kukamilishwa kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ulioanza mwaka 2018.

Rais pia aliagiza kuimarishwa kwa ulinzi kwenye miradi inayotekelezwa na Manispaa ya Morogoro kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuuungana na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kukamilisha barabara zilizoko kwenye mpango.

●**Imeandikwa na Christina Haule (MOROGORO) na Christina Mwakangale (DAR)**

# BoT yaagizwa utekelezaji riba za benki

**Na Benny Mwaipaja**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, ameiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) itekeleze haraka maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni kuhusu Taasisi za Fedha kupunguza riba za mikopo.

Rais Samia alisema lengo ni kuwawezesha wafanyabiashara na Watanzania kwa kukopa na kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Masauni alitoa maagizo hayo alipotembelea BoT Jijini Dar es Salaam na kufanya mazungumzo na uongozi wa benki hiyo ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kutembelea taasisi zilizochini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Alipongeza jitihada zinazofanywa na Benki Kuu ya Tanzania za kukutana na wadau ili kuhakikisha kuwa Taasisi za Fedha zikiwamo benki na watoa huduma wa Sekta Ndogo ya Fedha wanapunguza riba za mikopo yao ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo isiyo na gharama kubwa.

"Niwapongeze kwa juhudi zilizoanza kuchukuliwa kuwezesha riba kupungua na ikiwezekana mwishoni mwa mwezi huu wananchi waanze kuona matokeo ya juhudi hizo kwa riba kuanza kupungua, kwa kuwa kupungua kwa riba ni jambo linalowezekana," alieleza Mhandisi Masauni.

Aidha, ameitaka benki hiyo kuhakikisha inaweka mikakati mahususi ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kwa kuwa na mbinu za kibunifu zikiwamo kuanza kununua na kuhifadhi dhahabu pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa za Tanzania nje ya nchi na kusimamia kikamilifu shughuli za utalii.

Kuhusu suala la fedha za wananchi waliokuwa wateja wa Benki ya FBME Limited iliyowekwa chini ya uangalizi wa Bima ya Amana za Wateja inayosimamiwa na BoT ikiwa katika hatua za kufilisiwa, Masauni, ameitaka benki hiyo kuhakikisha wateja wake wanarejeshewa fedha zao haraka baada ya kukamilisha taratibu za kisheria zinazoendelea nchini Cyprus.

Naibu Gavana wa BoT, Dk. Bernard Kibesse, alimhakikishia Masauni kwamba Benki yake inakamilisha mazungumzo na benki ili washushe riba kama alivyoelekeza Rais Samia jijini Mwanza.

Alisema BoT pia inaendelea kurekebisha kanuni mbalimbali za mikopo inayotolewa na benki hiyo kwa benki ili kuziongezea ukwasi na zenyewe zitumie fursa hiyo kushusha riba za mikopo.

Alisema BoT itaanza kununua na kuhifadhi dhahabu baada ya kiwanda cha kuchakata dhahabu cha Mwanza kilichozinduliwa na Rais Samia jijini Mwanza hivi karibuni kupata hati ya uthibitisho ya uzalishaji wa dhahabu wa viwango vya kimataifa ambavyo ili cheti hicho kitolewe, kiwanda kinatakiwa kuzalisha dhahabu yenye ubora wa asilimia 99.9.

## Baba Mtakatifu ateua maaskofu wasaidizi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis amewateua Padri Henry Mchamungu na Padri Stephano Musomba, wa Shirika la Waagustiniani (O.S.A) kuwa maaskofu wasaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam kuanzia jana.

Taarifa ya uteuzi huo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima.

Taarifa hiyo ilimwelezea Askofu Mteule Mchamungu kuwa alizaliwa Januari 18, mwaka 1965, eneo la Legho Kilema Jimbo la Moshi, mkoani Kilimanjaro, na kwamba baada ya masomo yake ya upadri, alipewa daraja takatifu la upadri Juni 24, mwaka 1994.

"Alihudumu katika nafasi mbalimbali za utume Jimbo Kuu la Dar es Salaam na TEC, hadi uteuzi wake alikuwa Mwalimu na mlezi Seminari ya Segerea, Dar es Salaam," ilieleza taarifa ya Padri Dk. Kitima. Kwa mujibu wa Katibu huyo, Askofu mteule Musomba alizaliwa Septemba 25, mwaka 1969 eneo la Malonji Jimbo la Mbeya, na baada ya masomo ya upadri alipewa daraja takatifu la upadri Julai 24, mwaka 2003, na kuhudumu katika nafasi mbalimbali za utume shirikani na Jimbo la Dar es Salaam na Jimbo la Morogoro.

"Hadi uteuzi wake, Askofu mteule alikuwa Paroko wa Parokia ya Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Mavurunza, Dar es Salaam na Katibu wa Shirika lake la Waagustiniani Kanda ya Tanzania," ilifafanua taarifa hiyo.

HABARI KITAIFA

# TMDA yajitosa ubora wa chanjo ya corona

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imesema imeimarisha mifumo yake ya udhibiti kuhakikisha inafuatilia kwa ukaribu ubora, usalama na ufanisi wa chanjo ya corona itakapoingia nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya 45 ya Biashara Kimataifa, maarufu (sabasaba), mkoani Dar es Salaam.

Alisisitiza chanjo hiyo itakapowasili nchini, itahakikiwa na kusajiliwa ilivyo kwa chanjo na dawa zingine.

"Timu yetu ya wataalamu na mifumo yetu ipo vizuri kwa ajili ya kuzifanyia usajili chanjo, ni jukumu letu (TMDA) kuhakikisha chanjo hiyo inakuwa salama na inafaa kwa matumizi," alisema Fimbo.

Kuhusu usalama wa chanjo hiyo, Fimbo alisema kama ilivyo kwa chanjo zingine zozote, ikishapitishwa haimaanishi kwamba itatumika bila kusababisha athari kwa binadamu.

Alisema ni jukumu la mamlaka hiyo kuendelea kufuatilia kwa karibu madhara yanayoweza kuletwa na chanjo na dawa.

"Chanjo hii pia tumeiweka katika huu utaratibu, tutakapokuja kuiruhusu kutumika, tutaifanyia ufuatiliaji wa ukaribu ili kama kuna madhara yoyote yanatojitojeza tuweze kuyafahamu na kuchukua hatua haraka," alisisitiza Fimbo.

Kadhalika, alisema wataalamu wa TMDA tayari wameshiriki katika utafiti na tathmini ya chanjo hiyo kupitia nchi jirani za Jumuiya ya Maendeleo za Nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema TMDA kuwapo katika jopo hilo kunaisaidia nchi kuwa na uhakika wa kupata chanjo iliyo salama na kuishauri serikali namna ya kuitumia bila kuleta madhara.

"Tumeshiriki kuifanyia utafiti chanjo hiyo na mifumo tuliyoiweka tunaamini itakapoingia nchini itatunzwa vyema na kutumiwa salama," alisema Fimbo.



Kaimu Mganga Mfawidhi katika Hospitali ya Rufani ya mkoani Shinyanga, Dk. Mfaume Salum (kulia), akipokea msaada wa mitungi ya hewa ya Oksijeni 16, kutoka kwa Mwenyekiti wa klabu ya mazoezi Polisi Jamii Fitness, Sadick Kibira, mjini Shinyanga jana, kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wenye changamoto ya upumuaji. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mwanasaikolojia ataja kiini wanandoa kuuana

**Na Waandishi Wetu**

MAGOLANGA Shagembe, Mwanasaikolojia na Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ameanika kiini cha matukio ya kuuana miongoni mwa wachumba na wanandoa yanayoripotiwa kwa wingi nchini kwa sasa.

Shagembe ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Wanasaikolojia Tanzania (TAPA), alisema mkoani Dar es Salaam juzi kuwa tatizo hilo linachagizwa na uchumba na ndoa nyingi kujengwa kwa msingi aliouita mbovu wa kukidhi haja ya kimwili.

"Uhusiano unavunjika kwa sababu yanajengwa katika msingi mbovu. Vijana wengi wanaingia kwenye uhusiano kwa lengo la kukidhi haja zao za kingono tu, na si mapenzi ya dhati.

"Ili uhusiano uwe na tija, ni lazima kuwe na vitu vya ziada vya kuwaunganisha wahusika, tofauti kabisa na kuishia kufanya mapenzi tu. Mfano, kushauriana mambo ya shule, kazi na maisha kwa ujumla," alisema.

Mtaalamu huyo wa saikolojia alitoa angalizo kwamba mtu unayejenga naye uhusiano, anapaswa kuwa mke au mume mtarajiwa na si vinginevyo.

Katika hilo, alisema tatizo linalokumba vijana wengi sasa ni kuingia kwenye uhusiano kama sehemu ya starehe, yaani kukidhi haja za mwili tu na si vinginevyo.

"Ikumbukwe kwamba hakuna binadamu aliyekamilika asilimia 100, kukoseana na kugombana ni sehemu ya maisha ya uhusiano. Kinachopaswa kufanyika ni kuwa wepesi wa kuomba msamaha na wepesi wa kusamehe.

"Hata bila kuombwa msamaha, kusamehe ni kiungo muhimu kwenye ustawi wa penzi.

"Ili mapenzi yawe ya furaha, upendo na amani, ni muhimu kwa wahusika kujiandaa kikamilifu na kuwa tayari kimwili, kiakili, kihisia na hata kiuchumi pia.

"Kuingia katika uhusiano bila maandalizi ni mwanzo wa kufeli katika uhusiano. Linapotokea tatizo kwenye uhusiano, mfano kugombana, kila mmoja anatakiwa kuwa sehemu ya suluhisho na siyo kumtupia lawama mwingine, kulaumu hakujawahi kutatua tatizo, hivyo ni muhimu kuzungumza kwa pamoja na si kulaumu," alifafanua.

Ushauri wake kwa vijana ni watambue uhusiano ni mchakato, hivyo hakipaswi kuwa kitu kinachotokea ghafla kama ajali.

Alisema kuwa kabla ya kuanzisha uhusiano, ni vyema wakaanza na urafiki wa kawaida ili kupata muda wa kusomana hasa kimtazamo na kitabia.

"Katika urafiki, ukiona mitazamo na tabia za unayetaka kuwa naye kwenye uhusiano haziendani na za kwako au na kile unachotamani mwenzi wako awe nacho, ni ngumu kuishi naye kwa amani.

"Hivyo, wanatakiwa kufanya chaguo na kufikiria maisha yao ya baadaye na uamuzi huo utawaweka huru na katika hali ya amani," alisema.

Kumeshuhudiwa 'songombingo' la matukio ya wachumba na wanandoa kuuana nchini, vijana wanaosoma katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu wakiwa sehemu ya baa hilo.

Julai 18, mwaka jana, Jeshi la Polisi liliripoti tukio la mmoja wa wanafunzi katika Chuo cha Sayansi Mbeya (MUST) kudaiwa kumuua mchumba wake aliyekuwa anasoma naye chuoni huko kwa kile kilichodaiwa kuwa wivu wa mapenzi.

Vilevile, Juni Mosi mwaka huu, kuliripotiwa tukio kama hilo katika Chuo Kikuu cha Tumaini mkoani Iringa, wanafunzi wawili wa chuo hicho wenye umri wa miaka 21 na 22 wakitajwa katika tuhuma za kifo cha mmoja wao aliyeuawa kwa kunyongwa.

**●Imeandaliwa na Grace Masunga na Rehema Gohage, SJMC**


ÇELEBİ

Celebi Tanzania Aviation Services Ltd

## PRESS RELEASE

**Çelebi is expanding its global network in Tanzania**

Celebi Tanzania Aviation Services Ltd. which is a subsidiary company of Çelebi Aviation has been awarded a concession for the "Provision of Ground Handling and Cargo Services" at Julius Nyerere International Airport in Tanzania and started its operation as of 1st March, 2021.As Celebi Aviation; we are dedicated to provide excellence in ground handling services along with our ancillary products. Celebi stepped into the aviation industry with the establishment of Celebi Ground Handling in 1958 as Turkey's first privately-owned Ground Handling Services Company. Today, Celebi stands out as one of the most successful Ground Handling providers of integrated services in India, Budapest, Frankfurt and Turkey, offering a full range of services with over 13,000 dedicated employees, at more than 40 stations.

Our dedicated headquarters and operational teams are ready to carry our global quality in Tanzania with the support of the local leadership. Our operational start up team as well as ground support Equipment (GSE) are ready on ground for our valuable customers.

As a company, we are strongly motivated to go past the Covid-19 pandemic and keep our aim and focus on our planned growth in developing markets. Çelebi is confident that from our starting point in Dar es Salaam, we will continue to expand into other rapidly emerging aviation markets in Africa.

**Celebi Tanzania Aviation Services Ltd – "Rising Together"**

**For more information, please contact the undersigned.**
**Ferda Yakar**
**General Manager Tanzania**
**+255 745 601 992**
**ferda.yakar@celebiaviation.com**

116349202

MAHOJIANO MAALUM

# Mkurugenzi wa Tiba: Hii hapa mikakati yetu kuikabili corona

## ●Vikwazo viwili vyamuumiza kichwa

**Na Waandishi Wetu**

VITA dhidi ya ugonjwa wa Covid-19 imeshaanza rasmi nchini, wakati jana Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa Kibaigwa wilayani Kongwa, alitamka hadi sasa awamu mpya ya maradhi hayo ina wiki tatu.

Mnamo Juni 28 mwaka huu, Rais Samia aliweka wazi tayari kuwapo wastani wa wagonjwa 100 na kati yao, 70 walikuwa wanapumua kwa msaada wa mashine.

Kutokana na hatua hiyo, Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, wao wakiwa wenye dhamana, katika mazungumzo na Nipashe, amefafanua hatua wanazochukua kuirejesha nchi kwenye ahueni. Kwa namna gani?



Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi

**MAABARA ZA UPIMAJI**

Dk. Subi anasema suala muhimu wanalolifanya ni kuwa na maabara za kutosha za upimaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema walianza na maabara moja baadaye wakaongeza zingine lakini na sasa kuna vituo vingi katika kila mkoa vya kukusanyia sampuli ili kusafirisha kwenda kupima.

"Wizara tumesema tunataka kupanua wigo wa kuongeza maabara. Hasa badala ya kuwa nazo maabara mbili za Arusha na Dar es Salaam, tunataka tuongeze maabara Kanda ya Ziwa moja ya upimaji pia Dodoma, na tumeshafanya tathmini ya awali na utaratibu unaendelea kuhakikisha tunakuwa na maabara," anasema.

Dk. Subi anasema lengo la kuwa na maabara za kutosha ni kuhakikisha wanasogeza huduma karibu na wananchi ili kupunguza adha ya kusafirisha sampuli umbali mrefu.

Anasema tayari walishaanzisha upimaji katika viwanja vya ndege, mipaka yote kwa lengo la kuimarisha na utambuzi na wanapima vinasaba vya virusi vya corona ili kuona ubadilikaji wake.

Anasisitiza kuwa eneo hilo wamelipa kipaumbele kikubwa katika kuhakikisha watu wanapata huduma stahiki na kwa wakati.

Kadhalika, anasema wanahakikisha kusiwe na ucheleweshaji wa majibu na wananchi wapate huduma stahiki katika eneo la maabara na upatikanaji wa maji na sabuni za kunawia uwe wa uhakika katika maeneo hayo.

Anasema pia wameweka mkakati wa kutoa msaada wa saikolojia kwa ndugu wa watu waliopoteza maisha kutokana na janga hilo ili wasahau na kuendelea na maisha mengine.

Dk. Subi anasema huduma hiyo itatolewa katika ngazi zote na wanawashirikisha viongozi wa dini katika kuhakikisha wanapata elimu ya kutosha.

**URATIBU**

Mtaalamu huyo wa afya anasema uratibu unaendelea pamoja na utafutaji wa rasilimali na tayari serikali na wadau mbalimbali wameendelea kujitokeza kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Anasema wananchi na watu binafsi na mashirika ya kimataifa bado wanaendelea kujumuika na wizara katika kuhakikisha wanadhibiti ugonjwa huo nchini.

Anasema wanaendelea na uratibu wa kuimarisha wataalamu wa ndani wakiwamo watumishi wa afya ili kuhakikisha wako imara katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Hili linaenda sambamba na kuhakikisha katika maeneo yote muhimu kwenye vituo vyetu vya huduma kwenye maeneo ya mipakani tunakuwa na rasilimali ya kutosha katika kukabiliana na ugonjwa huu.

"Lakini tunashukuru kwamba uratibu huu siyo katika ngazi ya taifa tu pia katika ngazi ya mikoa wameandaa mipango mikakati ambayo inaiandaa kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huu," anasema.

**UDHIBITI WA MIPAKA**

Anasema pia wameimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa ugonjwa huo katika maeneo yote, yakiwamo ya mipakani kwa kuanzisha huduma ya upimaji wa corona.

"Sisi tunachokifanya katika maeneo ya mipakani hatupimi tu corona, tunapima na maradhi mengine ili kuhakikisha wanakuwa salama.

"Tunapokuta na maradhi, tunawaweka karantini kwa siku 14 kuhakikisha wanakuwa sawa kabla ya kwenda kujichanganya na wengine," anafafanua.

Anasema wamekuwa na utaratibu wa kuelimisha umma kupitia mitandao ya kijamii, runinga na nyumba kwa nyumba katika mitaa ili kuelewa na kutokuwa na hofu ya aina yoyote.

"Tunapoenda kutembea nyumba kwa nyumba, tuwaambia kabisa wasipaniki kwa sababu ugonjwa huu umekuwapo kwa muda sasa, lakini tunawaomba sana wananchi wasiupuuze kwa sababu corona ni ugonjwa na tumeshuhudia vifo vikitokea," anasema.

Dk. Subi anasema wanahimiza wananchi wachukue tahadhari na kufuata hatua zote za kujikinga kama kuvaa barakoa kwa usahihi katika maeneo ya mikusanyiko.

Anasema pia wanawahimiza watu kunawa mikono mara kwa mara kwa maji safi tiririka na sabuni au vipukusi.

Anasema wanasisitiza watu kunawa mikono kwa sababu watu walirudi nyuma hivyo wanapaswa kuendelea na utaratibu huo.

"Tunasema kwamba ni vizuri na kusisitiza sana maeneo yote ya umma na binafsi katika makanisa na misikiti watu watumie vipukusi, lazima tuhakikishe utamaduni wa kimila unazingatiwa, unaweza kukuta mtu ameshika meza mwingine akashika wakaambukizana," anasema.

**MAKUNDI MAALUM**

Dk. Subi anasema wanatoa elimu kwa watu wenye magonjwa sugu kama shinikizo la damu, moyo na wazee ambao wapo katika hatari ya kupata maambukizi.

"Na kwa bahati mbaya sasa hivi aina mpya ya virusi vya corona inaathiri watu wa rika zote, hata wa umri chini ya miaka 60," anasema.

VIKWAZO

Dk. Subi anabainisha vikwazo katika kukabiliana na ugonjwa huo ikiwamo watu kulalamika kuwa chanjo ni mbaya ilhali dunia inaendelea kupata chanjo.

Anasema hadi sasa, kupitia WHO, watu bilioni moja wameshachanjwa na maeneo mengine wanaendelea kutoa chanjo kwa ufanisi mkubwa na watu wanaendelea vyema na majukumu yao.

Anasema kwa Afrika uchanjaji uliofanyika ni mdogo, ukiwa chini ya asilimia mbili, idadi ambayo ni sawa na kwamba bara halijachanja watu wake.

"Na ndiyo maana hapa tunasema kama nchi ni vizuri tukasema tunaanza kuimarisha uzalishaji wa chanjo ndani ya Afrika.

"Tuzalishe wenyewe, hili ni jambo la msingi, tumeona mataifa makubwa pia wamechukua chanjo karibia mataifa 10, mataifa mbalimbali duniani yamechukua asilimia 10 na mengine kama 10 tu na mengine, zimekuja kwa hiyo unaweza kuona kuna suala la tatizo la kiuchumi," anafafanua.

Dk. Subi anasema Waafrika wanapaswa kuendelea kuungana ili kujenga teknolojia imara na nzuri ambayo pia itasaidia nchi za Afrika kujitegemea.

Anasisitiza kuendelea kuelimisha wananchi kuwa Tanzania siyo wageni katika kutoa chanjo, wakianza tangu mwaka 1970 kwa kutoa chanjo kama polio na surua.

"Sasa chanjo hii ya corona watu wanasema 'kwa nini imefanyika haraka haraka?' Siyo chanjo ya kwanza kutolewa haraka haraka, duniani zipo chanjo zingine ambazo tunaweza kutengeneza na kuanza kutolewa zikaleta matunda, kwa hiyo ipo haja ya wananchi kuelimishwa," anasema.

Dk. Subi anasema kikwazo ni upatikanaji wa rasilimali kama vifaa tiba katika hospitali zote nchini.

Anasema wanahitajika wataalamu wa kutosha, vyumba maalum vya wagonjwa mahututi, vitanda na upatikanaji wa gesi tiba.

Anarejea kuwa hivi karibuni Waziri wa Afya, alizindua mitambo saba mipya ya kuzalisha Oksijeni ambayo kila mmoja una uwezo wa kuzalisha mitungi 200 kwa siku.

**MIONGOZO**

Dk. Subi anasema serikali ilitengeneza miongozo katika wimbi la kwanza na la pili, hivyo wanaendelea kuipitia ili kuhimiza utekelezaji wake. Anasema wanataka kuweka miongozo kwenye shule, michezo, viwanja vya ndege na mahali penye mikusanyiko ili watu waifuate wakati wa kutekeleza shughuli zao.

Anaitaka jamii kutopuuza ugonjwa huo, bali kuzingatia elimu inayotolewa na wataalamu wa afya kuachana na habari zisizo sahihi za kwenye mitandao na kama kuna mwenye tatizo, apige simu kwa namba 199 ili kupata msaada.

**●Imeandaliwa na Mary Geofrey, Renatha Msungu na Edwin Mosha (TURDACO)**

# Samia ateta na bosi wa Barrick

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kuzungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni za Barrick Gold, Mark Bristow Ikulu jijini Dodoma.

Mazungumzo hayo, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema hayo yalihusu masuala mbalimbali ya utendaji kazi wa kampuni hiyo na kampuni ya Twiga.

Katika mazungumzo hayo, taarifa hiyo ilisema Bristow alimhakikishia Rais Samia kuwa Barrick itaendelea kushirikiana na serikali katika uwekezaji wa Sekta ya Madini nchini na iko tayari kuendelea kuwekeza katika maeneo mengine.

Alisema wanaendelea vizuri na mfumo wa makubaliano baina yao na serikali katika kuhakikisha pande zote mbili zinanufaika na rasilimali ya madini nchini.

Aidha, Bristow alisema kwa sasa Barrick imeajiri Watanzania wengi ikiwa ni pamoja na uongozi wa juu wakiwamo Mkurugenzi Mtendaji, Meneja Mkazi na Mkuu wa Hesabu.

Mtendaji huyo mkuu aliongeza kuwa Barrick imefanya maboresho ya usimamizi wa mazingira katika mgodi wa North Mara ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa kuhifadhi na kutibu maji yanayotokana na uzalishaji wa madini.

Pia alisema kwa sasa Barrick imeongeza ushiriki wa Watanzania katika kutoa huduma mbalimbali katika migodi yake na kwamba kakriban asilimia 70 ya bidhaa inazotumia ni kuitoka kwa Watanzania.

Kwa upande wake, Rais Samia alimhakikishia mwekezaji huyo kuwa serikali yake itaendelea kushirikiana nao kwa kutekeleza yale yote waliyokubaliana kwa lengo la kuhakikisha rasilimali ya madini inanufaisha pande zote mbili kwa manufaa ya taifa.

Aidha, Rais Samia alimshukuru Bristow kwa utayari wake wa kushirikiana na serikali katika kukabiliana na ugonjwa wa corona nchini.

# CCM yaishukuru China ujenzi Chuo cha Uongozi

**Na Beatrice Shayo,** KIBAHA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema msaada wa ujenzi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere nchini na Serikali ya China utakwenda kuwajengea uwezo viongozi wa vyama vya siasa wa ndani na nje ya nchi.

Ujenzi huo ulianza mwaka 2018 baada ya vyama sita vya siasa ambavyo vilishiriki wakati wa mapambano ya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika zikiwamo CCM, ANC, ZANU PF, FRELIMO, SWAPO na MPLA.

Chongolo aliyasema hayo wakati wa sherehe za kuanzishwa kwa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) wakiadhimisha miaka 100 ambayo ilikutanisha nchi 100 na marais 23 katika mkutano uliofanyika kwa mtandao (Zoom) wakiwamo wanachama wa CCM.

Chongolo alisema ushiriki huo siyo wa bahati mbaya umeasisiwa na viongozi wakuu, Mao Ze dong na Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1963. "Uhusiano kati ya CCM na CPC umekuwa ukiongezeka siku hadi siku na uhusiano huu umeimarishwa na kutembelewa na viongozi kutoka pande zote mbili," alisema.

Alisema Tanzania inajivunia kuonyesha miradi ya kihistoria ambayo imetekelezwa nchini Tanzania kwa msaada wa China chini ya uongozi wa CPC pamoja na reli ya TAZARA inayounganisha Tanzania na Zambia.

Alitoa mfano wa kiwanda cha Urafiki cha Dar es Salaam akisema jina hilo lilitokana na urafiki kati ya China na Tanzania.

Naye Rais wa China, Xi Jinping alisema chama hicho kimepiga hatua kutokana na ushirikiano na vyama vingine katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Jinping ambaye ni kiongozi wa CPC alisema chama chake hakiwezi kukua bila kushirikiana na vyama vingine na kazi yao ni kuleta maendeleo kwa wananchi na kujali haki za watu.

Alisema kuna haja ya kufanyakazi na kushughulikia changamoto zinazoikabili dunia pamoja na janga la Uviko ambalo limeleta machafuko makubwa duniani.

Alisema hakuna haja ya kulaumiana kuhusu janga hilo badala yake wakae pamoja na kutafuta suluhu.

Jinping alisema mapambano dhidi ya janga la Uviko, yanahitaji ushirikiano wa vyama na nchi nyingine, CPC itaendelea kusaidiana katika kutokomeza ugonjwa huo.

Alisema kila nchi ina haki ya kuamua jinsi ya kupata demokrasia yake badala ya kunyoosheana vidole.

Alisema watu wa nchi zote wana chaguo la kuchagua njia yao wenyewe kuelekea demokrasia na sio kuiga nchi kwa uamuzi wake.

Kwa upande wake Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema hafla hiyo imewafurahisha watu wengi siyo kwa China pekee bali ulimwenguni.

"Tuko hapa leo tunawakilisha harakati za dunia kwa ujumla tukiwa na lengo moja la amani na mshikamano," alisema Rais Ramaphosa.

Ramaphosa alisema kama Waafrika wanathamini sera zilizowekwa na china kwa ajili ya maendeleo ya pamoja kwa Afrika na kwamba China imekuwa rafiki mwaminifu kwa nchi nyingi za Afrika.

Alisema kuna haja ya umoja, mshikamano na upendo ili kuweza kuvuka mpaka uliopo kati ya maskini na matajiri kwenye suala la upatikanaji wa huduma za dawa na vifaa vya matibabu katika ugonjwa wa Uviko.

Alisema nchi zinahitaji kufanyakazi kwa pamoja kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma kwenye suala la upatikanaji wa chanjo ya ugonjwa huo.

Alisema dunia inatakiwa ipige vita suala la utaifa kwenye suala la upatikanaji wa chanjo bila kufanya hivyo hawatapiga hatua dhidi ya vita ya corona duniani.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KUITWA SHAURINI MDAIWA

Mahakama ya Mwanzo MAKOLE
Wilaya DODOMA

MADAI NAMBARI 33/2021

MDAI UNAMBWE SAMWEL NASSARI

DHIDI YA

MDAIWA DEVOTHA STEPHANO MLINGI

KWA DEVOTHA STEPHANO MLINGI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TALAKA(KUACHANA).

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Ijumaa tarehe 16/07/2021 saa 08:00 asubuhi.
kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **06/07/2021.**

116349002




Muuguzi wa Hospitali ya KAM Musika ya Kimara Korogwe, mkoani Dar es Salaam, Happy Thomas (kushoto), akitoa maelezo kwa wageni kuhusu huduma zinazotolewa na hospitali hiyo kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yanayoendelea kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE DISTRICT /RESIDENT MAGISTATE'S COURT OF MUSOMA AT MUSOMA

RM CIVIL CASE NO 08 OF 2014

MAFURU D MAGANILA..............D/HOLDER
VS
MAKIRE AUCTION &ANOTHER........J/DEBTOR

*Notice to show cause why execution should not issue (order xxi,rule 20(1) of the civil procedure code)*

To: Juma Hassan ebambo
P o box 339
Musoma

Whereas the* plaintiff/defendant has made application to this court for execution of decree in the above suit on the allegation that the said decree has transferred to him by assignment or without assignment),this is to give you notice that you are to appear before this court on 12nd ,day of july,2021 at 08:00 hrs to show cause why execution should not be granted.

**Given under my hand the seal of the court this 23rd day of june 2021**

Resident Magistrate

J/Debtor

116348602


# Mongella akoshwa na uwekezaji kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amesema uwekezaji uliofanywa na Kampuni ya Mbolea Yara Tanzania, unakwenda kubadilisha maisha ya wakulima nchini, ikiwamo mnyororo wa thamani katika ukuaji wa uchumi.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa programu connect itakayotumiwa na wakulima kupata taarifa mbalimbali kidigitali, Mongella alisema elimu hiyo italeta mabadiliko makubwa mkoani humo, ambao sehemu kubwa ya wakazi wake wanategemea kilimo na ufugaji.

Aidha, alisema uwekezaji uliofanyika katika sekta hiyo unakwenda sambamba na jitihada za serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuinua uchumi kupitia uwekezaji sekta ya kilimo.

"Naipongeza kampuni ya Yara katika kuendelea kubuni mbinu za kidigitali ili kujiweka karibu na wakulima, tunapoizindua programu hii ni matumaini yetu kama serikali kwa wadau wote watatumia 'App' hii vizuri kwa malengo ya kupata ufanisi na maendeleo katika kilimo chetu hapa Arusha," alisema na kuongeza;

"Wakulima wakipata elimu ya kutosha wataongeza uzalishaji na kuingia kwenye kilimo cha biashara, tutajitosheleza kwa chakula na malighafi ya viwanda vya kuchakata mazao, halmashauri zitapata mapato ya kodi, hii itasaidia sana kukua kwa uchumi wa Arusha na kwa nchi yetu kwa ujumla."

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya Yara Tanzania, Winstone Odhiambo, alisema imekuwa mstari wa mbele kubuni mbinu sahihi za kilimo kwa kutumia njia za kidigitali ili kuongeza upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wakulima.

Naye Meneja Masuluhisho ya Kidigitali wa Yara, Deodath Mtei, alisema sasa wakulima wa mazao mbalimbali mkoani Arusha wanaweza kuwa na uhakika wa kupata matokeo bora ya kilimo wakifanyacho, kutokana na taarifa za kitaalamu zinazopatikana katika programu mpya ya yara connect iliyozinduliwa mkoani humo.


KUPOTEA KWA CHETI



**LAMECK NYAMBAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0144-0054** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NSUMBA SEKONDARI** mwaka 1998. Yeyote atakayekionা atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/338224/2021.**

116349302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Oksijeni iongezwe haraka hospitalini

**JUZI** Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, jijini Mwanza imesema inakabiliwa na uhaba wa mitungi 500 ya kuhifadhia oksijeni kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wenye matatizo ya upumuaji, wakiwamo wa corona.

Hospitali hiyo ina mitungi 100 inayotumika kwa siku, huku mahitaji ya mitungi 300 na kuwaomba wadau kutoa msaada ili ipatikane mitungi 500 inayotosheleza mahitaji kwa idadi ya wagonjwa hospitalini hapo.

Alisema idadi ya wagonjwa wanaofika hospitalini wanaohitaji mitungi ya oksijeni ni wengi, na kwamba mahitaji yanaongezeka, huku ikiuzwa ghali na kushauri kuwapo kwa wazalishaji wengi na uzalishaji kwa wingi ili ishuke bei na kuwezesha upatikanaji wake kwa urahisi.

Kwa sasa serikali imethibitisha kuwapo kwa wimbi la tatu la corona, na kwa mujibu wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuna wagonjwa kama 100 na kati yake 70 walikuwa wanapumulia mashine, na kwa sasa tahadhari inachukuliwa ikiwamo kuhakikisha uvaaji wa barakoa kila wanapokuwa kwenye mikusanyiko.

Jana Rais Samia akiwa Kibaigwa mkoani Dodoma kwenye ziara ya kikazi, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari zote muhimu kwa kuwa wimbi la tatu la corona lipo nchini na hata Dodoma lipo, ambalo ni hatari zaidi, jambo ambalo linadhihirisha zinahitajika tijihada za mtu mmoja mmoja, jamii na mamlaka kutoa elimu kwa umma ili kutoa tahadhari.

Hii ni hospitali moja katika ya nyingi zilizopo nchini, ambayo imeeleza wazi uhaba wa mitungi hiyo, hivyo nidhahiri kuwa kutokana na kuthibitika kuwapo kwa corona, idadi ya wanaohitaji kutumia oksijeni inaweza kuongezeka, jambo ambalo linahitaji hatua kuhakikisha inapatikana. Tunaamini serikali ikijipanga vyema na wadau wengine itakuwa rahisi kukabili wimbi hili na madhara hayatakuwa makubwa kama ilivyotokea kwenye nchi nyingi. Wale waliojiandaa mapema walifanikiwa kukabili wimbi hilo kiasi cha kutoleta madhara, na wapo ambao wameshaacha kuvaa barakoa.

Tunaamini serikali na wadau wa afya wamesikia kilio cha hospitali hiyo, za rufani, teule, za mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati, ili kusaidia kuboresha huduma za afya, hasa kwa wakati huu, na pale inapowezekana kuwa na mitungi ya oksijeni iwepo ya kutosha.

Hili ni muhimu kutokana na ukweli kuwa tunaona kwenye nchi za Uganda, Zambia na Afrika Kusini ambako zimezidiwa na corona kiasi cha hospitali kuzidiwa na oksijeni kutotosha mahitaji, hivyo kusababisha wengi kupoteza maisha wakati ingewezekana kwa kupata huduma sahihi za afya.


Ni muhimu mamlaka husika hasa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kushirikiana na wadau wa sekta binafsi kuchangia mitungi hiyo na kuhakikisha inasambazwa kwenye hospitali zote za serikali au zinazoendeshwa kwa ubia kati ya serikali na taasisi za dini.

Hii ni namna mojawapo ya kujipanga kukabiliana na kusambaa ikiwamo kuokoa maisha ya wananchi ambao watahitaji huduma hiyo kwa ukaribu zaidi, isisubiriwe hospitali zikishaelemewa wagonjwa ndipo mitungi hiyo iongezwe.

Tunaona ni muhimu serikali ikawa inatoa takwimu za hali ya ugonjwa huo ikiwa njia ya kuwafanya wananchi kuona ni hatari, kwa kuwa kwa sasa watu wanakwenda kwenye mikusanyiko bila kuchukua tahadhari, na hilo linaonekana kwenye masoko, sherehe, maeneo ya biashara na nyumba za ibada.

Bila kuwa na mitungi ya kutosha kuna hatari ya ugonjwa huo kusambaa kwa kasi, na kupoteza watu muhimu, ambao maisha yao yangeokolewa, kwa kuwa kabla ya wimbi hilo kulikuwa na mahitaji ya mitungi hiyo, uwepo wa wimbi umeongeza mahitaji ambayo ni lazima kuangalia mwelekeo na kuboresha. Maandalizi ni muhimu ili kukabiliana na hali yoyote inayoweza kujitokeza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani hili linatosha kuhamia kulinda afya



Na Sabato Kasika

**KILA** kampuni inayotengeneza sigara, kwa sasa imeweka maandishi kwenye pakti yanayosomeka hivi; 'Onyo uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya yako', kwa lengo la kuwakumbusha wavutaji kulinda afya zao.

Onyo hilo linatokana na kwamba uvutaji wa tumbaku una madhara mengi ambapo wataalamu wa afya wanasema, sigara ina kemikali zaidi ya 4,000 ambazo zina uwezo wa kudhuru afya ya binadamu.

Kutokana na hali hiyo, watu wanatakiwa kuwa makini na ndio maana wakawekewa maandishi ya onyo, licha ya kwamba baadhi ya wavutaji hawatilii maanani onyo hilo kwa usalama wa afya zao.

Onyo hilo lingetosha kuwafanya wavutaji kujiongeza na kuachana na tumbaku kwa ajili ya kulinda afya zao, badala ya kusoma onyo hilo kisha kuliacha lilivyo na kumbe lina umuhimu.

Sigara ni moja ya bidhaa pekee ambayo watumiaji wanapewa tahadhari kuhusu madhara ambayo wanaweza kuyapata iwapo watautumia, hivyo umuhimu wa kujiongeza na kuachana nayo ni mkubwa.

Chama cha Kudhibiti Matumizi ya Tumbaku Tanzania (TTCF), kilishawahi kutoa taarifa kuwa utafiti unaonyesha kwamba asilimia 32 ya saratani zote zinasababishwa na uvutaji wa tumbaku (sigara).

TTCF inasema, utafiti huo ulifanywa na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) mwaka 2009, maeneo ya mijini tu na kwamba huenda vijijini hali ikawa mbaya zaidi.

Madhara ya tumbaku ndio ambayo hivi karibuni yaliwaibua wataalamu wa afya kutoka Hospitali Muhimbili-Mloganzila kutoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Salma Kikwete iliyopo Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Janet Komba alisema, matumizi ya tumbaku yanaathiri mfumo wa fahamu wa binadamu.

Kwamba, katika tumbaku, kuna kichocheo kiitwacho nikotini ambacho kinafanya mtu ajione kama ana nguvu nyingi, hivyo kupenda kuitumia mara kwa mara na kumbe anadhuru afya yake.

Alikumbusha kuwa, wakati wa kuanza uvutaji kunakuwa na changamoto nyingi ikiwamo kukohoa, kichwa kuuma, mapigo ya moyo kwenda mbio na kujihisi kuumwa lakini mtu akishazoea inakuwa vigumu kuacha kuvuta.

Dk. huyo anabainisha kuwa ugumu wa kuacha tumbaku unatokana na kichocheo kilichopo kwenye kilevi hicho, na kwamba, kuvuta tumbaku kila wakati kuna athari kubwa kiafya.

Miongoni mwa athari hizo ni kupata magonjwa mbalimbali yakiwamo kiharusi, mshtuko wa moyo, saratani ya koo na mdomo, ambapo njia pekee inayoshauriwa ni kuachana ni matumizi ya tumbaku.

Elimu ambayo imekuwa ikitolewa na wadau wa afya juu ya madhara ya tumbaku pamoja na onyo ambalo limewekwa kwenye pakti za sigara vina umuhimu mkubwa katika kuokoa afya za Watanzania.

Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu, wavutaji na wasiovuta kuwa makini kwa ajili ya kulinda afya zao, kutokana na kwamba hata asiyevuta anaweza kuathirika moshi wa sigara kutoka kwa mvutaji.

Mazingira ambayo watu wengi wameyazoea ni ya kuchanganyika na wavutaji, hivyo si ajabu mvutaji akawasha sigara na kuanza kuvuta kwenye mkusanyiko wa watu bila kujali kwamba anadhuru wasiovuta.

Vilevile si ajabu kukuta mtu yuko ndani ya gari na familia yake huku akivuta sigara, au mtu amembeba mtoto huku akivuta bila kujali kwamba anamuumiza kwa moshi wa sigara anaotoa.

Pamoja na hayo, ni muhimu kuzingatia maelekezo mbalimbali ya wataalamu wa afya, kwa kutambua kuwa uvutaji wa tumbaku ni hatari, ingawa baadhi ya wavutaji hudai kwamba, hiyo ndio starehe yao hawawezi kuiacha.

Nimalizie kwa kukumbusha kuwa, taarifa iliyowahi kutolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), ni kwamba, gharama za magonjwa yatokanayo na matumizi ya tumbaku kila mwaka ni dola trilioni 1.4 kote ulimwenguni.

# Nishati, mawasiliano vinara mashauri Baraza la Ushindani

**Na Mwandishi Wetu**

SEKTA za Nishati na Mawasiliano zinaongoza katika mashauri ya rufani yanayotolewa na Baraza la Ushindani (FCT).

Katika mashauri ya rufani 215 kati ya 250, sawa na asilimia 86 yaliyowasilishwa katika kipindi cha mwaka 2015 hadi mwaka huu, yanatoka kwenye sekta hizo.

Mshauri wa Sheria wa Baraza la Ushindani (FCT), Kunda Mkenda, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la baraza hilo lililoko ndani ya banda la Wizara ya Viwanda na Biashara katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara (DITF), maarufu Sabasaba, yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Alisema FCT imetoa uamuzi katika mashauri ya rufani 215 kati ya 250 sawa na asilimia 86 yaliyowasilishwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2021.

Pia alisema FCT imepata mafanikio hayo, licha ya mrundikano uliokuwapo baada ya muda wa wajumbe ambao ni miaka mitatu kumalizika.

"Kuna kipindi muda wa wajumbe ulikuwa umemalizika, hivyo kukawa na mrundikano wa mashauri. Lakini sasa wameteuliwa tayari na wataanza kazi hivi karibuni," alisema.

FCT ambayo mwenyekiti wake ni Jaji wa Mahakama Kuu anayeteuliwa na Rais, ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoanzishwa na serikali ili kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za rufani.

Rufani hizo ni zile zinazotokana na uamuzi wa Tume ya Ushindani (FCC) na Mamlaka za Udhibiti kama Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga (TCAA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Mkenda aliwahimiza watu kutembelea banda hilo ili wajue haki zao wanapokuwa wanapata na kutumia huduma mbalimbali zikiwamo za ununuzi na utumiaji wa nishati, mawasiliano na usafiri wa anga na ardhini.

"Baraza limepewa hadhi ya kimahakama ya utoaji haki katika masuala ya ushindani, udhibiti wa soko na kumlinda mtumiaji wa huduma. Uamuzi wa kesi za rufani na za maombi unaotolewa na Baraza la Ushindani ni wa mwisho," alisema.

Licha ya rufani za mashauri hayo kutoka katika sekta za nishati, mawasiliano, usafiri wa anga na ardhini sambamba na rufani zinazotokana na ushindani katika soko, alisema mashauri mengi kati ya hayo yalihusu hasa sekta ya nishati kupitia EWURA na mawasiliano kupitia TCRA.

Mkenda alisema mafanikio hayo yameongeza uwajibikaji katika upangaji bei za nishati ikiwamo ya umeme na usafiri huku kampuni zikiongeza umakini kwa kufuata sheria sambamba na kuongezeka uwazi na ushindani wa bei katika kampuni za simu na uwajibikaji kwenye ushindani katika sekta ya biashara.

Akizungumzia malengo ya kimkakati ya FCT kwa mwaka 2021- 2022, Mkenda alisema ni kuanza kutekeleza mpango mkakati mpya wa 2021/22 hadi 2025/26 baada ya uliopo kumalizika Juni, mwaka huu.

"Mingine ni kuboresha mazingira na kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri. FCT imejipanga kuboresha mifumo inayotumika katika usikilizwaji wa mashauri ikiwamo ya kurekodi, kufungua na kusajili mashauri kwa njia ya mtandao."

**"Kuna kipindi muda wa wajumbe ulikuwa umemalizika, hivyo kukawa na mrundikano wa mashauri. Lakini sasa wameteuliwa tayari na wataanza kazi hivi karibuni," alisema.**

# 30 wachuana kumpata Mwenyekiti NACONGO

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO), leo linatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu ngazi ya taifa baada ya kukamilisha ngazi za wilaya na mkoa.

Katika uchaguzi huo, jumla ya wajumbe 30 kutoka mikoa yote nchini, wanatarajiwa kushiriki kumpata mwenyekiti, katibu mkuu na mweka hazina.

Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Uchaguzi wa Baraza la NACONGO, Wakili Flaviana Charles, akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Dar es Salaam kuhusu uchaguzi huo, alisema unatarajiwa kufanyika mjini Dodoma.

Alisema baada ya uchaguzi huo, kesho viongozi waliopatikana wataapishwa na Julai 10 watakabidhiwa ofisi na nyaraka kutoka kwa viongozi waliopita.

Akizunguzia vikwazo vilivyopo, Wakili Flaviana, alisema baadhi ya wagombea walikosa sifa kwa sababu ya asasi zao kutosajiliwa na wengine kutofuata masharti ya uendeshaji wa asasi ikiwamo kulipa ada.

Alisema wajumbe wengine walishindwa kushiriki uchaguzi huo kwa kukosa rasilimali fedha za kufika wilayani na wengine walitaka kushiriki bila kushirikisha asasi wanazosimamia.

Kuhusu viongozi watakaochaguliwa, Wakili Flaviana aliwahakikishia kuzingatiwa kwa makundi maalum kama watoto, vijana, watu wenye walemavu na kundi la mashirika ya kimataifa.

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TRA KUKUTANA NA WADAU WA FILAMU NCHINI**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itakutana na wadau wa Filamu nchini siku ya **tarehe 10 Julai, 2021** kwa ajili ya kujadili kodi mbalimbali zinazogusa mazao ya filamu ikiwemo Kodi ya Zuio (Withholding Tax) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Katika kikao hicho, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itakuwepo kutoa ufafanuzi juu ya sera ya matangazo ya biashara kwenye chaneli za kulipia (Pay TV).

Aidha, Bodi ya Filamu Tanzania ikiwa ni Taasisi inayosimamia Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini itahudhuria kama mlezi wa tasnia hiyo.

Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Chuo cha Kodi (ITA) **P.O.Box 9321, Mikocheni Dar es salaam Tel: +255 22 2216800/1** au **+255 783081348 Email: ita@tra.go.tz kuanzia saa 7:00 mchana.**

Wadau wote wa filamu nchini wanakaribishwa.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

# Chongolo aonya viongozi wapenda utukufu

**Na Jacqueline Liana**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema uongozi siyo ukubwa wa kutaka utukufu, bali ni wajibu unaoambatana na dhamana.

Amekemea tabia aliyoita ya ovyo ya baadhi ya wana-CCM ya kupanga safu za uongozi kinapofika kipindi cha uchaguzi wa viongozi.

Aliyasema hayo jana katika Wilaya ya Sumbawanga Vijijini, Mkoa wa Rukwa, ambako yuko kwa ziara ya kikazi katika mikoa ya Rukwa, Mbeya na Songwe, akiwa amefuatana na wajumbe wa Sekretarieti ya CCM Taifa, Komredi Ngemela Lubinga, Komredi Shaka Hamdu Shaka na Komredi Kenani Kihongosi.

Chongolo alikuwa akizungumza na viongozi na watendaji wa CCM wa mkoa huo katika kikao kilichofanyika Sumbawanga Vijijini, na kufafanua kwamba, lazima kila kiongozi ajiulize amewafanyia nini wale anaowaongoza.

"Ukiwa kiongozi lazima ujiulize nini umekitendea chama na wanachama, ukiitwa mwenyekiti siyo kwa sababu ya shati ulilovaa au viatu ulivyopiga kiwi au mtindo wa nywele ulionyoa," alionya Chongolo.

"Uongozi ni wajibu wa kujua ni kipi chenye maslahi kwa chama," alisema na kunukuu kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwamba "uongozi ni mzigo".

Alisema kwamba mwaka 2022 ni wa uchaguzi ndani ya CCM na ni wakati wa kuwapata viongozi bora na siyo wale wanaopangwa kwa maslahi binafsi.

Pia, alisema miongoni mwa wana-CCM kuna wanaofaa kuwa viongozi, lakini hawana kimbelembele kama wale wanaondekeza upangaji wa safu.

Alisema wanachama wenye sifa za kuwa viongozi hapana budi washawishiwe wagombee nafasi za uongozi katika chama.

Akimnukuu Mwalimu Nyerere, Chongolo alitaka wanaokimbilia uongozi kuogopwa kama ukoma.

"Eti kuna mwingine anajipanga kuwa kiongozi...niwaombeni mhakikishe hamruhusu watu wanaopanga safu. Watu wazuri hawana tabia ya kimbelembele kutaka madaraka," alisema.

Aliitaja kazi nyingine na viongozi ni kuwaandaa viongozi wa baada yao, kwa sababu uongozi ni kupokezana vijiti.

"Mtu huwezi kuwa kiongozi milele," alisema na kuhoji kwanini mtu ang'ang'anie madaraka?

# Aibuka na gari 'SimBankin Mzigo Promosheni'

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imemkabidhi gari mshindi wa kwanza wa kampeni ya "SimBanking Mzigo Promosheni," Kelvin Ngao.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Stephen Adili, alisema mshindi huyo amepatikana kwa kufanya miamala mingi zaidi kupitia huduma ya SimBanking.

"Kampeni yetu inalenga kuwahamasisha wateja kujenga utamaduni wa kutumia mifumo ya kidijitali ikiwamo SimBanking kufanya miamala yao. Tumekuwa tukitoa zawadi ya Sh. 100,000 kwa wateja wetu wenye miamala mingi zaidi kila siku na leo hii tunakwenda kutoa zawadi ya gari kwa mshindi wa jumla wa mwezi Juni, Kevin Ngao," alisema Adili.

Alisema katika kampeni hiyo CRDB pia inatoa elimu kwa wateja wake ya matumizi ya huduma ya SimBanking na wateja wamekuwa wakiulizwa maswali kupitia mitandao ya kijamii na radio na kujishindia zawadi ya Sh. 30,000. Mpaka sasa benki hiyo imeshatoa jumla ya Sh. milioni 15 kwa washindi 500.

Akielezea mafanikio ya kampeni hiyo alisema katika kipindi cha mwezi Juni matumizi ya huduma ya SimBanking yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 20 kutokana na uelewa wa wateja ya urahisi na unafuu wa kupata huduma.

Adili alisema kampeni hiyo pia imezaa matunda katika upande wa elimu ya kufungua akaunti kupitia SimBanking App na hadi sasa zaidi ya wateja 30,000 wameshafungua akaunti kupitia mfumo huo wa kidijitali.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi wa shindano hilo, Ngao aliishukuru CRDB kwa zawadi hiyo ya gari huku akibainisha siri ya ushindi ni kujenga utamaduni wa kutumia SimBanking kufanya miamala yake.

"Ninafurahia sana kufanya miamala kupitia SimBanking iliyoboreshwa, imekuwa rahisi na nafuu sana kutumia. Sasa hivi miamala yangu yote nakamilisha kupitia SimBanking, iwe kufanya malipo kupitia CRDB Lipa Namba, kutuma pesa, kulipia bima, kulipia kodi na kutoa fedha kwa CRDB Wakala/ ATMs na tawini bila ya kadi," alibainisha Kevin.

Meneja wa Biashara Kanda ya Mashariki, George Yatera, alimpongeza mshindi huyo pamoja na washindi wengine wote waliopata zawadi kupitia kampeni hiyo huku akitoa rai kwa wateja wengine wa benki hiyo kushiriki kampeni kwa kuendelea kufanya miamala kupitia huduma hiyo.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Benki ya CRDB, Stephen Adili, akimkabidhi zawadi ya gari mshindi wa kampeni ya SimBanking "Mzigo Promosheni," Kevin Ngao. Wengine pichani ni Mkuu wa Kitengo cha CRDB Wakala (wapili kushoto), Ericky Willy na Meneja Biashara Kanda ya Mashariki, George Yatera. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tume ya Madini, TANTRADE zapigwa jeki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa Sh. milioni 50 kulipia gharama za ukarabati wa banda la Tume ya Madini na Bodi ya Biashara ya Nje katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba).

Maonyesho ya mwaka huu yamevutia zaidi ya kampuni 3,000 za ndani na nje tangu yalipoanza Juni 28 mwaka huu na yanatarajiwa kufikia tamati Julai 13, 2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordinson, alifafanua kampuni yake imeamua kutoa kiasi hicho cha fedha ukiwa ni mwendelezo wa msaada wake kwa Tume ya Madini kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita.

Aliongeza kuwa kaulimbiu ya mwaka huu ambayo ni "Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu", inakuja wakati mwafaka wakati nchi inaendelea kuimarisha hali ya uchumi baada ya kuingia katika kundi la uchumi wa kati.

"Kama mshirika, GGML imekuwa mfano wa kuigwa na kuwa sehemu ya mipango ya serikali kuwanufaisha raia wake kwa kulipa kodi mbalimbali ikiwamo ushuru wa huduma na mrabaha. Tangu miaka mingi GGML imeonyesha ushirikiano wa dhati kwa Tume ya Madini kwa kuzingatia sheria na kanuni za madini," alisema Jordinson.

Alisema GGML ni kampuni ya kwanza ya uchimbaji madini nchini kutekeleza ipasavyo mpango wa uwajibika kwa jamii kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2017.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa GGML itaendelea kufanya kazi na serikali na wadau wengine kufikia na kuvuka lengo la sekta ya madini kuchangia asilimia 10 kwa Pato la Taifa (GDP) ifikapo mwaka 2025.

Kampuni hiyo inajitahidi pia kushirikiana na serikali za mitaa na jamii pia katika utambuzi na usimamizi wa miradi muhimu ambayo itasaidia mustakabali endelevu wa kijamii na kiuchumi kwa wilaya.

# Mwanakijiji ashinda zawadi gari mil. 169/-

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mkoa wa Morogoro, Abdallah Mohammed, kukabidhiwa zawadi ya gari la kifahari aliloshinda lenye thamani ya Sh. milioni 169.

Ameshinda zawadi hiyo katika promosheni ya Benki ya NMB ya Bonge la Mpango, ambayo ilimalizika jana.

Gari hilo aina ya Toyota Fortuner alilolinyakua mshindi huyo kutoka kijiji cha Kinole ni jpya ambalo lilianza kutembea kilomita zake za kwanza jana baada ya mshindi huyo kuliendesha akiwa na familia yake kuelekea nyumbani baada ya shughuli ya makabidhiano.

"Hatimaye sasa nimeamini kuwa mimi ndiye kweli mshindi wa zawadi kubwa ya shindano hili ingawa nilipata taarifa ya ushindi wangu katikati ya mwezi jana," mwanakijiji huyo mwenye umri wa miaka 50 na mzazi wa watoto watano alisema baada ya kuliwasha gari hilo.

Aliipongeza NMB kwa mikakati yake wezeshi kama kampeni ya Bonge la Mpango ambayo uzinduzi wake ulifanyika mwanzoni mwa mwaka huu.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, alisema zawadi zilizonyakuliwa ni pamoja na pesa taslimu walizoshinda wateja 120. Nyingine ni pikipiki za miguu mitatu 24 aina ya LIFAN na Kirikuu tatu za muundo wa TATA Ace.

Meneja wa Tawi la Uluguru, Lilian Abraham, alisema ana sababu kubwa mbili za kufurahia ushindi wa Abdallah ambazo ni mshindi huyo kuwa mwanakijiji na kubwa zaidi kuwa mteja wa tawi lake.

# Shirika kuwanoa waraghabishi

**Na Happy Severine,** MASWA

WARAGHABISHI 36 kutoka vijiji 18 wilayani Maswa mkoani Simiyu, wanatarajia kupatiwa mafunzo kupitia mradi wa uraghabishi utakaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Social Development Foundation.

Watapatiwa mafunzo ya kuwajengea stadi za uraghabishi na kuwawezesha kufanya shughuli hizo katika ngazi ya vijiji vyao kwa kushirikiana na serikali.

Akizungumza katika uzinduzi wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Shirika la Kawiye Social Development Foundation, Ezekiel Kassanga, alisema ili kufikia malengo, mradi utatoa mafunzo hayo ambayo yatawawezesha moja kwa moja waraghabishi kushirikiana na viongozi wa serikali katika kutumia mifumo iliyo ya pamoja na mbinu bunifu ili kufikia malengo ya pamoja.

Kassanga alisema katika mradi huo wananchi nao watashirikishwa kwa njia ya mikutano na majadiliano.

# PUMA sasa kuwaunganisha Watanzania utafutaji petroli

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), imesema imejipanga kuwaunganisha Watanzania katika shughuli za utafutaji wa petroli.

Shughuli hizo ni zinazohusisha ushiriki wa wazawa (local content) katika kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa na huduma za ndani ya nchi.

PURA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji (EWURA) imesema imeandaa kanzi data itakayoanza kufanya kazi Julai 15, mwaka huu ili kuwapata watoa huduma wazawa na kuwaunganisha na wageni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangwen, alisema jukumu hilo linatokana na umuhimu wa kuwaandaa Watanzania kufanya kwa kina shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi zaidi ya ilivyo sasa.

Alisema watahakikisha wanawajengea uwezo na kuwapa taarifa sahihi kuhusu kuongeza mnyororo wa thamani wa bidhaa na huduma zao na kuchangamkia fursa katika miradi inayotekelezwa na kampuni kubwa kwa usimamizi wa PURA.

Sangweni alisema Watanzania wana fursa katika usafirishaji, vyakula na ushiriki wa kazi hizo kwa kuajiriwa na kuwa mbia. Ubia ni takwa la lazima ambapo wazawa wanashirikiana na kampuni za kigeni kwa asilimia 25.

Mkuu wa Kitengo cha Ushiriki wa Wazawa na Uhusishwaji wa Wadau wa PURA, Charles Nyangi, alisema kanzi data itawaunganisha watoa huduma wazawa na wageni ambapo kila kampuni ya kigeni ya kutafuta na kuchimba mafuta na gesi itapaswa kuwapata watoa huduma katika kanzi data hiyo.




Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mohamed Moyo (wa tatu kushoto), akiagana na Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, Brighton Gavile, baada ya mazungumzo alipofika kwa ajili ya kujitambulisha juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Shule yapokea matundu 20 ya vyoo

**Na Christina Mwakangale**

BENKI ya TPB imesaidia kuondoa tatizo la vyoo kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Ifwagi katika kijiji cha Ifwagi, Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa na kuwapatia matundu 20 ya vyoo.

Mkuu wa Shule hiyo, Imani Nyoni, akisoma risala ya shule wakati akikabidhiwa majengo yenye matundu ya vyoo, alishukuru TPB kwa kuwaondolewa tatizo la uhaba wa vyoo vilivyokuwa haviridhishi kutokana na yaliyosababisha athari kubwa kiafya kwa wanafunzi pamoja na walimu.

"Shule yetu ina wanafunzi wasiopungua 211 ambao wote walikuwa wanategemea matundu machache sana ya vyoo wakati wakiwa shuleni," alisema.

Alibainisha kuwa shule hiyo kwa muda wa kipindi kirefu walikuwa wakijaribu kuomba wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa majengo mapya ya wanafunzi pamoja na walimu pasipokupata mafanikio.

Kadhalika alisema ilibidi bodi ya shule iweze kufanya kikao na wazazi, walezi pamoja na wanakijiji mbalimbali waweze kununua vifaa mbalimbali vya ujenzi ili kujenga kwa nguvu zao wenyewe.

"Katikati ya mchakato huo ndio tukapata wafadhili wetu kutoka Benki ya TPB ambao kiukweli ni wadau wakubwa sana kwenye elimu na kusaidia hadi leo hii tupo hapa tunakabidhiwa majengo haya."

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TPB, Diana Myonga, alisema, TPB imekabidhi majengo ya matundu 20 ya vyoo yenye thamani ya Sh. milioni 56.2 kwa ajili ya shule hiyo.

Myonga aliongeza kuwa pia TPB wameahidi kutoa msaada wa samani za ofisi za walimu, ambazo shule iliomba kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wao akisema msaada huo ni sehemu benki hiyo kurudisha faida kwenye jamii kutokana na kuiunga mkono benki hiyo.

# Dangote kuongeza uzalishaji saruji nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANDA cha kuzalisha saruji cha Dangote kimesema kitaendelea kuongeza uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu kwa ajili ya ujenzi ili kuendana na mahitaji yanayokua kwa kasi katika soko la Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdullahi Baba, alisema saruji inayotengenezwa na kampuni hiyo imepokelewa vyema na Watanzania na kuongeza kuwa mahitaji yamekuwa yakiongezeka kwa kasi.

Alisema tangu kiwanda hicho kianze kufanya kazi mwaka 2015, kimekuwa kikijikita katika kutengeneza bidhaa bora, lakini zenye gharama nafuu, lengo likiwa pia ni kuwawezesha Watanzania kumiliki nyumba.

« Kumekuwapo na uwekezaji mingi na mikubwa ya miundombinu Tanzania, na Dangote tumekuwa ni moja kati ya wazalishaji wakubwa kuliko wengine wote wa saruji kwa ajili ya miradi hii. Tunayo furaha kutoa mchango wetu katika maendeleo ya miundombinu kwa Tanzania.»

Alisema Dangote inaona Tanzania kama sehemu muhimu ya biashara yake kutokana na hatua mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuweka mazingira bora ya uwekezaji ambayo yanaipa nguvu kampuni hiyo kuendelea kuwekeza.

Tumeshaanza kuongeza uzalishaji wetu na tutaendelea kuongeza zaidi na zaidi kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na saruji ya kutosha. Mazingira ni rafiki na tunapenda kuuhakikishia umma kuwa Dangote ipo na itaendelea kuwapo,» aliongeza.

Alisema Dangote Cement pia ina mipango ya kuzalisha saruji na kuiuza katika siku za usoni na kuongeza kuwa kiwanda hicho kina uwezo mkubwa wa kuzalisha saruji kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Saruji ya Dangote Tanzania, Abdallahi Baba, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu bidhaa zinazozalishwa na kampuni hiyo, katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# VETA ilivyokuza taaluma ya ufundi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), imesema kufanya kazi na wenye viwanda kumesaidia kwa kiwango kikubwa kukuza taaluma ya ufundi stadi nchini na hata kuchochea ubunifu zaidi kwa wakufunzi.

Akizungumza jana katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yanayofanyika viwanja vya Julius Nyerere, Mwenyekiti wa Bodi ya VETA, Peter Matiku, alisema mamlaka hiyo iligundua kwamba kuna faida kubwa kufanya kazi na wenye viwanda kutokana na aina ya wataalamu wanaowazalisha kutoka katika vyuo vyao.

Alisema katika kipindi cha maonyesho wamejipanga kuonyesha bunifu zao mbalimbali ikiwamo maabara inayotembea, ambayo itaondoa changamoto kubwa katika shule ambazo hazina maabara hadi sasa.

"Tumejipanga kuongeza uchumi katika sekta ya viwanda hasa kwa vijana wanaonza vyuo na hata waliopo kazini tayari," alisema Matiku.

Alisema hata wafanyakazi waliopo kazini kwa muda mrefu wanaruhusiwa kwenda VETA kwa ajili ya kupata mafunzo mbalimbali ili kuongeza tija katika kazi zao.

Mkurugenzi Mkuu wa VETA, Dk. Pancras Bujulu, alisema katika maonyesho ya mwaka huu, mambo mengine ambayo wamejipanga kuonyesha ni bidhaa za mikakati ikiwamo vifaa vya kilimo, viwanda na ufugaji.

Alisema VETA imejiimarisha zaidi katika utoaji wa elimu kwa kuongeza vyuo 33 katika mikoa kadhaa na kufanya kuwa na jumla ya vyuo 71.

Dk. Bujulu alisema bunifu zao zinaongeza ufanisi zaidi katika jitihada za uchumi wa viwanda, ambao Tanzania imeulenga.

# CTI yataka sera nzuri ulinzi viwanda vya ndani

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini (CTI), limeomba serikali kuendelea kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuweka sera nzuri ili viendelee kukua kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kutengeneza ajira kwa Watanzania.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Shirikisho hilo, Leodgar Tenga, wakati akizungumza na wabunge wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

Tenga alisema viwanda vya ndani haviogopi ushindani wa bidhaa kutoka nje ya nchi, lakini bidhaa hizo zisipo dhibitiwa na kulipa kodi ipasavyo upo uwezekano wa kuviua viwanda vya ndani na kuwakosesha vijana wengi ajira.

Alisema mataifa yote duniani yanalinda viwanda vya ndani lengo likiwa ni kulinda ajira za wananchi wake hivyo serikali ya Tanzania inapaswa kuiga mataifa hayo.

"Hatuogopi ushindani na wala hatusemi kwamba kusiwe na ushindani na wenzetu wa nje kwa sababu bila ushindani viwanda vyetu vitabweteka lakini tunachoomba tusiviache tu bila ulinzi maana kupambana na maviwanda makubwa kazi kweli," alisema Tenga.

Mbunge wa Bihalamuro Magharibi (CCM), Ezra John, naye aliunga mkono hoja ya kuvilinda viwanda vya ndani ambavyo vimeajiri mamilioni ya Watanzania na kwamba kufa kwake kutasababisha kuyumba kwa uchumi.

Alisema viwanda vya ndani kwa muda mrefu vimekuwa vikilalamikia utitiri wa kodi hivyo serikali inawajibika kuangalia namna bora ya kuzipunguza ili kuviondolea mzigo.

Ezra alisema wabunge na wadau mbalimbali wanapaswa kuangalia chanzo cha sheria hizo zinazolalamikiwa na kama bado zinapaswa kuendelea kuwapo au zifanyiwe marekebisho.

"Unaweza kukuta kuna mfanyabiashara alifanya makosa ikatungwa sheria ambayo inawabana watu wengi sasa lazima tujue sheria fulani inayolalamikiwa ilianzia wapi na kwasababu gani ili kama haina maana tena kwa wakati huu tuachane nayo," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Erick Shigongo, alisema serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara, hivyo wenye viwanda nao wanapaswa kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi kwa uaminifu.

"Serikali hii inawalinda wafanyabiashara na wenye viwanda kwa kuweka sheria na sera nzuri, lakini nyinyi CTI muwakumbushe nao kwamba wanapaswa kuwa waaminifu kwa kutii sheria za nchi hii," alisema.

ama
ALHAMISI JULAI 8, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Dk. Ama: Afya tunajipanga kwa elimu corona kwa angalizo 'kuna kujisahau'**



Ukurasa 12

Tishio ongezeko unene kupita kiasi



Ukurasa 14

**Utamaduni, tamaa wazazi zinawatwika mimba wanafunzi, ndoa nyingi utotoni**

# Namna ilivyo chanjo corona na hatua kinga mpya shuleni

**Na Yasmine Protace**

VIRUSI vya ugonjwa wa corona, vinaendelea kuwa kero katika umma, tiba, kuugua na mengine mengi. Tiba ya kwanza inatajwa ni kwa kila mmoja kuchukua tahadhari stahiki ya kujilinda.

Katika kuhakikisha ugonjwa huo unadhibitiwa, serikali imeshaanza mchakato wa kutengeneza chanjo ya virusi vya corona nchini, ili kupunguza gharama ya uagizaji nje ya nchi na kuzifanya ziwe karibu na wananchi walioko.

Prof. Abel Makubi, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anasema kiwanda kitakachojengwa hakitaishia kuzalisha chanjo pekee za dawa hizo, pia dawa za kutibu magonjwa mengine.

"Wataalamu tunao wengi na kiwanda hicho hakitatengeneza chanjo ya UVIKO 19 pekee, hata ikiisha tutaendelea kuzalisha chanjo nchini," anasema Prof. Makubi, anayefafanua kwamba, hakutaruhusiwa kuingizwa chanjo hizo kinyume na utaratibu utakaowekwa.

Prof. Makubi anawataka viongozi na wasimamizi wa shule, kuzingatia mwongozo wa kudhibiti UVIKO 19, ili isiathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

Anasema, wakati shule na baadhi ya taasisi za vyuo zimeshaanza masomo wiki hii, mwongozo utakaotumika ni uliotumika mwaka jana, ila umepitiwa upya kuendana na mahitaji ya sasa.

Katibu Mkuu anasema serikali inawakumbusha viongozi wa taasisi za elimu, kuboresha mifumo ya malezi mabweni, kupitia ukaguzi na ufuatiliaji wa kila mara afya za wanafunzi.



Aina ya hatua za kujihami dhidi ya corona kwa wanafunzi shuleni. **PICHA: MTANDAO.**

"Mambo muhimu ni viongozi wa shule na vyuo kuandaa miundombinu ya maji na upatikanaji wa barakoa kama ilivyokuwa mwaka jana," anasema Prof. Makubi.

Aidha, anasisitiza elimu ya kujikinga iendelee kutolewa kwenye maeneo kama nyumba za ibada, shuleni na vyuoni.

**NAIBU KATIBU MKUU**

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Elimu, Prof. Carolyne Nombo, anasema watashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), itasimamia miongozo hiyo iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

"Miundombinu yote ifufuliwe, ikiwamo matumizi ya vitakasa mikono, barakoa asilia na maji yanayotiririka," anaainisha na anairodhesha ya kuzingatiwa yanajumuisha uwapo wa vifaa vya kunawa mikono vyenye maji tiririka, sabuni au vitakasa mikono vya usafi binafsi

Ni nyenzo anayotaja inapaswa kuwapo katika kila darasa, ofisi, geti, lango kuu, bweni, maktaba, bwalo la chakula, vyoo na maeneo mengine muhimu ya mkusanyiko huo wa watu.

Aidha, kuna msisitizo walimu na wakufunzi wanapaswa wapewe elimu juu ya kuzingatia yanayozuia maambukizi ya Covid -19 katika maeneo ya kazi, kabla ya kufunguliwa shule, vyuo na taasisi.

"Vituo vyote vinatakiwa viwe na dawa na vifaa kwa ajili ya dharura. Wataalamu wa afya wa halmashauri wafanye ukaguzi katika shule, vyuo na taasisi za elimu ili kuhakikisha tahadhari zote za kujikinga na maambukizi ya COVID-19 zimezingatiwa," anasema.

Hoja nyingine ya wizara husika, ni kwamba walimu wa afya na malezi wapatiwe elimu ya utoaji msaada wa kisaikolojia kuwasaidia wanafunzi, walimu na wafanyakazi katika eneo husika wakiwasiliana na wataalamu wa afya walioko jirani.

Kuna rai kwa uongozi wa shule, vyuo na taasisi za bweni zihakikishe kunakuwapo na nafasi ya kutosha (mita moja) kati ya kitanda na kingine bwenini, kudhibitiwa uchangiaji vifaa kwa wanafunzi kama vile taulo, mashuka, vyombo vya usafi wa mavazi na mwili.

Prof. Carolyne, anasema uongozi wa shule, vyuo na taasisi ziweke utaratibu mzuri wa upatikanaji barakoa katika maeneo yao, kwa gharama nafuu.

Aidha, anaunganisha na haja ya jamii kuhamasisha wazazi na walezi kuwapatia watoto wao barakoa na kuhakikisha walimu na wafanyakazi wote wanavaa barakoa muda wote wa kazi.

Watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wenye magonjwa ya moyo, selimundu (sickle cell) mfumo wa hewa kama vile pumu na matatizo mengine ya kiafya hawaruhusiwi kuvaa barakoa.

"Uongozi wa vyuo na shule utatakiwa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kuhifadhia taka zitokanazo na barakoazilizotumika na kuziteketeza kama taka nyingine hatarishi," anasema.

Jamal Jabel, mkazi wa jijini Mwanza anasema kuwa serikali imefanya jambo jema kujenga kiwanda kwa ajili ya chanjo.

Anasema kuwapo kwa kiwanda hicho kitaisaidia hata serikali kutoagiza dawa nje na pia matumizi ya pesa yatakuwa sio makubwa kwa kuwa dawa itazalishwa hapa nchini.

Habiba Juma anasema elimu iendelee kutolewa, baadhi ya watu bado hawana mwitikio wa kuvaa barakoa .

Anasema watu wanakuwa katika mikusanyiko, unakuta mikusanyiko hiyo waliovaa barakoa wachache, sasa hapo inaonekana wasiovaa barakoa elimu watakuwa hawana.

Anasema anaipongeza serikali kwa kuandaa mwongozo katika shule na vyuo, maana kipindi hiki ndio wanafunzi wamefungua shule hivyo watajilinda.

***Makala nyingine ukurasa 12***

AFYA

# Dk. Ama: Afya tunajipanga kwa elimu corona angalizo letu 'kuna kujisahau'

## •Barakoa, maji tiririka... kituo afya muhimu

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeruhusu chanjo ya ugonjwa corona kusambazwa bure katika taasisi za umma na binafsi, ikitoa mwongozo wa kinga katika taasisi za elimu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Profesa Abeli Makubi, anasema kuna hatua nyingi na madhubuti zinaendelea kuchukulia kudhibiti wimbi la tatu la Covid-19, ikiwamo ujenzi wa kiwanda.

Hadi sasa jitihada zilizofanywa na serikali, ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu mlipuko wa ugonjwa huo mpya wa corona, dalili zilielezewa pamoja na namna ya kuepuka maambukizi.

KINACHOFANYIKA WIZARANI

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa Wizara ya Afya, Dk. Ama Kasangala, anaiambia Nipashe kuwa serikali inajipanga kuhakikisha wanadhibiti kuenea kwa ugonjwa huo.

Anasema wanatoa elimu hiyo kwa jamii, katika kudhibiti ugonjwa huo kwa makundi mbalimbali, yakiwamo ya viongozi wa dini, akiwaeleza ni muhimu kwa sababu wanawakilisha waumini na kwenye vikao washiriki kuwapa elimu, vipeperushi na miongozo ya afya.

"Kundi la wanahabari linahusika sana katika kuelimisha namna ya kuripoti kuhusu corona, kwa hiyo wanafanya vikao kwa ajili ya kuzungumza nao namna bora ya kuwafikisha taarifa kwa jamii," anasema.

Dk. Ama anafafanua kuwa wanatengeneza machapisho mbalimbali kwa kulenga watu na makundi ya kama wasiyoona na wasiyosikia.

**WENYE ULEMAVU**

Upande wa ufikishaji wa taarifa sahihi kwa makundi maalum nchini, Dk. Ama anasema wanashirikiana na Chama cha Walemavu Tanzania, katika kupata maelezo ya namna ya kufikisha taarifa katika kundi hilo.

Anasema, wameshatengeneza kitabu kinachoelezea dalili za corona na namna inavyoambukiza na kinga yake kabla ya kuendelea kuenea nchini.

"Tayari tumeshachapisha kitabu kimoja cha nukta nundu kwa ajili ya wenzetu wenye ulemavu wa macho ili wapate taarifa kamili ya kujikinga na corona," anasema Dk. Ama.

Anafafanua kuwa wanatoa elimu pia kwa watumishi wa afya ngazi ya jamii ambao wanakutana na wananchi mara kwa mara.

Kwa mujibu wa Dk. Ama, watoa huduma za afya wanajengea uwezo wa kutambua dalili za ugonjwa, namna ya kujikinga na kutoa elimu kwa jamii, akiwa na ufafanuzi:

"Watoa huduma za afya hasa vijijini wao wanapita katika maeneo yenyewe mikusanyiko ya watu kama kwenye vituo vya mabasi, masoko na kwenye mikusanyiko ambako wanapita kutoa elimu kwa jamii."



Namna ilivyo vita dhidi ya corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Mwananchi asiseme ana corona kwa sababu ya dalili ulizo nazo, hivyo mgonjwa anapaswa kwenda kwenye kituo cha afya, kwa ajili ya kupimwa na kupewa ushauri,"**

**KITUO CHA TAARIFA**

Anaeleza kuwa wanafanya kazi ya kutoa elimu kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa na wana kituo cha kupokea taarifa chenye watumishi 40 wa Sekta ya Afya katika ngazi mbalimbali, wakiwamo wauguzi, madaktari na wafamasia.

Dk. Ama anaeleza kwamba katika kituo hicho, wanapokea na kuorodhesha maswali yanayoulizwa kila mara, kwa lengo la kutoa majibu kupitia matangazo, ili mteja anapopiga simu ayasikie kabla ya kurudia kuuliza.

Anasema, pia wanatumia mitandao ya kijamii inayotumika kutoa elimu kwa jamii, kupitia kurasa zao za mitandao kama 'facebook, instagram,' na 'twitter.'

**MAPOKEO CORONA III**

Dk. Ama anasema, wapo kwenye mpango wa kukamilisha taratibu za kutoa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo, elimu hiyo itagusa makundi yote na umuhimu wa chanjo, ili kusaidia taifa kuepuka kupoteza watu kwa maradhi hayo.

Anasema lengo ni kuwapa elimu Watanzania kuondokana na dhana potofu kuhusu chanjo inayoenezwa na watu wasiyo na uelewa wa kutosha.

Pia, anasema ujio wa wimbi la tatu la corona ulipoingia nchini, mapokeo yalikuwa madogo na wananchi bado hawana kasi kubwa ya kukabiliana nayo kama hatua ya kuvaa barakoa.

Kwa mujibu wa Rais Samia Suluhu Hassan, aliposimama eneo la Kibaigwa wilayani Kongwa jana, alisema maradhi ya corona wimbi jipya lipo nchini kwa wastani wa wiki ya tatu sasa na tahadhari inapaswa kuchukuliwa.

Mwelimishaji Ana, anasema wimbi la tatu ni tofauti na yaliyotamgulia, kwa sababu linagusa makundi yote ya jamii; wazee, vijana na watoto.

Dk. Ama, anasema, kwa kuzingatia ukubwa wake, watoto wadogo wanapaswa kukingwa kwa kuepushwa na mikusanyiko na tayari wizara inayohusika na afya, imeshatoa mwongozo wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa, kujihami na maambukizi shuleni.

Anasema, pia kuna mwongozo wa vyombo vya usafiri, kuwakinga abiria.

**MAISHA YA TAHADHARI**

Dk. Ama analalamika kuwa bado hakuna hatua kubwa ya kuwapo maeneo ya kunawa mikono yanayojitosheleza. Anaendelea: "Awali ofisi na familia zilikuwa zimetenga ndoo na sabuni milangoni kwa ajili ya watu kunawa mikono, lakini kwa sasa ndoo zimetolewa na hakuna kunawa mikono."

Anasema, watu waliondoa ndoo na sabuni kwa sababu ya kutulia kwa wimbi la pili la corona, lakini sasa wanapaswa kuzirejesha na Dk. Ama, anasema hivi sasa wanaangalia sehemu zinazofaa kuweka miundombinu ya kudumu ya kunawa mikono.

"Katika kila ofisi na nyumba, ijengwe eneo la kunawa mikono, ili uwe utaratibu wetu kunawa mikono bila kusubiri taarifa za ugonjwa," anafafanua Dk. Ama.

**TIBA ASILI?**

Kuhusu tiba za asili, Dk. Ama anasema Watanzania wanaruhusiwa kuendelea nazo, ila Wizara ya Afya inaendelea na jitihada za utafiti wa viwango vyake.

Hiyo anasema, inaendana na kuzihimiza jamii kuzingatia lishe bora, kwa sababu kuna vyakula vinavyosaidia kupandisha kinga za mwili.

Anasema tiba ya asili peke yake haitoshi pasipo kujikinga au kuponyesha ugonjwa wa corona na kwamba dalili zote za corona zinafanana na magonjwa mengine mengi.

"Mwananchi asiseme ana corona kwa sababu ya dalili ulizo nazo, hivyo mgonjwa anapaswa kwenda kwenye kituo cha afya, kwa ajili ya kupimwa na kupewa ushauri," anasema Dk. Ama.

Kadhalika, anaonya watu kubweteka na tabia ya unywaji dawa za kupunguza maumivu pindi wanaposikia kuumwa, kwa sababu dawa hizo zinatuliza dalili za maradhi na kuibuka tena baadaye. Anashauri watu wanavyojisikia vibaya, wajieleleze kwenye vituo vya afya.



AFYA

# Tishio ongezeko unene kupita kiasi

Na Mwandishi Wetu

TISHIO la unene kupita kiasi na magonjwa yasiyoambukiza linazidi kuongezeka duniani kote.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2016 asilimia 39 ya watu wazima duniani, yaani watu bilioni 1.9 walikuwa na uzito uliopitiliza wakati asilimia 13 (watu milioni 650) walikutwa na unene kupita kiasi. Pia Watoto wapatao milioni 41 wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa na uzito mkubwa au unene kupita kiasi.

Utafiti mpya unaonesha watu wenye unene kupita kiasi wanaongezeka nchini, hali yenye hatari ya kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza kama vile kisukari na shinikizo la moyo. Utafiti huo unaonyesha kwamba hilo linaweza kuzidisha ukubwa wa bajeti ya kuhudumia afya za wagonjwa hao na kuathiri uchumi wa watu binafsi, familia na serikali.

Taarifa ya Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF) inashauri serikali iingilie kati haraka kwa kuchukua hatua ya kisera kudhibiti mwenendo huo ambao inasema unahusika na kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukiza.

Utafiti huu ni wa kwanza Afrika Mashariki na wa pili barani Afrika, baada ya ule uliofanyika Afrika Kusini, unaoangalia uhusiano baina ya sera za kifedha (kupitia ushuru) na sera za kiafya, hususani namna ushuru unavyoweza kudhibiti ulaji wa bidhaa zenye madhara kiafya.

Licha ya kuongezeka kwa vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza, inakadiriwa kwamba wenye magonjwa hayo wanatumia gharama za tiba na nyinginezo kwa wastani dola za Kimarekani 1,211.78 kwa mwaka kila mmoja. Aidha, utafiti umegundua hasara zingine zinazotokana na magonjwa hayo, kama vile upotevu wa mapato pale mgonjwa mwenyewe na wale wanaomhudumia mgonjwa wanaposhindwa kufanya kazi.

Gharama kwa serikali katika kuwahudumia wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza ilikuwa karibu maradufu kutoka dola za Kimarekani milioni 142.7 mwaka 2015/16 hadi dola milioni 280.6 mwaka 2019/20.

Utafiti huo wa taasisi ya washauri mabingwa, umeonesha kuwa idadi ya watu wazima wenye uzito uliopitiliza iliongezeka kutoka asilimia tano mwaka 2008 hadi asilimia 8.4 mwaka 2016, huku vifo vilivyotokana na magonjwa yasiyoambukiza vikichangia theluthi moja ya vifo vyote.

Tatizo la unene kupita kiasi liliripotiwa kuwa juu zaidi kwa wanawake (asilimia 12.7) kuliko wanaume (asilimia 4.1) na linaathiri zaidi kundi la umri wa miaka 45 - 54. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na namna mipango ya bajeti ya afya ambayo hujishughulisha zaidi na huduma za tiba kuliko zile za kinga inaelezwa kuwa sababu za kuongezeka kwa magonjwa hayo.

Utafiti huo ulioongozwa na Prof. Fortunata Makene, Mkuu wa Idara wa Utafiti wa Kimkakati na Machapisho wa ESRF, ulionyesha kuwa asilimia 97 ya bajeti ya taifa ya huduma za afya ilitumika kuwahudumia wenye magonjwa yasiyoambukiza na asilimia tatu tu ilienda katika kudhibiti magonjwa hayo.



Mazoezi ni njia mojawapo ya kuepuka unene kupita kiasi kama inavyoonekana katika picha tofauti. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**



> **“Tayari kuna kodi ya vinywaji vinavyonogeshwa na sukari. Marekebisho yanayopendekezwa ni yale ya kuongeza kiwango cha kodi kuliko kuleta kodi mpya,” inasema taarifa hiyo.**



Unene kupita kiasi ni mkusanyiko wa mafuta uliokithiri mwilini, unaotokana na ulaji wa mara kwa mara wa vyakula na vinywaji vyenye kalori nyingi.

Utafiti huo, uliofadhiliwa na Kituo cha Utafiti wa Maendeleo ya Kimataifa cha Canada (IDRC), umejengwa juu ya hoja za kitafiti zilizobainisha kuwa utumiaji wa vinywaji vinavyonogeshwa na sukari huchochea kuongezeka kwa uzito wa mwili. Watu wenye unene kupita kiasi huwa kwenye hatari zaidi ya kupata magonjwa yasiyoambukiza, kama vile matatizo ya moyo, kisukari na saratani mbalimbali.

Pamoja na kutaka zichukuliwe hatua mtambuka za kisekta kuhimiza ulaji wa vyakula visivyo na madhara kiafya na ufanyaji mazoezi, utafiti huo unapendekeza ongezeko la ushuru wa vinywaji vinavyonogeshwa na sukari kama soda na juisi ulio sawa na asilimia 20 ya bei za viunywaji hivyo, kama hatua ya kisera ya kuhinisha ulaji wake.

“Tayari kuna kodi ya vinywaji vinavyonogeshwa na sukari. Marekebisho yanayopendekezwa ni yale ya kuongeza kiwango cha kodi kuliko kuleta kodi mpya,” inasema taarifa hiyo.

Utafiti huo ulibainisha kuwa utozaji vinywaji vitamu ushuru zaidi unaweza kupunguza kuenea kwa tatizo la unene kupita kiasi kwa asilimia 6.6 kwa ujumla. Watafiti wanapendekeza kuwe na mashauriano na watengenezaji wa vinywaji hivyo, walaji na wadau wengine juu ya pendekezo kuhakikisha utekelezaji jumuishi.

Taarifa hiyo inasema matumizi ya ushuru kudhibiti ulaji wa bidhaa zenye madhara kiafya yamefanikiwa kwenye nchi nyingi, zikiwamo Afrika Kusini, India, Brazil, Denmark, Ufaransa, Uingereza na Bulgaria.

Utozaji wa kodi kwenye vinywaji vinavyonogeshwa na sukari sio tu kuwa utaimarisha hatua nyinginezo za kudhibiti unene kupita kiasi lakini utaongeza mapato ya serikali kwa ziada ya shilingi bilioni 452 kwa mwaka.

AFYA

# Utamaduni, tamaa wazazi zinawatwika mimba wanafunzi, ndoa nyingi utotoni

- Mahari ng'ombe zawatia viwewe wazazi
- Ushawishi wao mkuu 'jifelisheni watoto'



Mkurugenzi wa Shirika la Kiwohede linalotekeleza mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa Halmashauri ya Msalala, Justa Mwaituka, akieleza jambo kuhusu kupambana na ukatili kwa wasichana, kwa kuwapatia elimu ya ufundi. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

Ni kilio sasa wazazi na walezi wasiokuwa waadilifu katika kata 18 zinazounda Halmashauri za Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wanawazuia mabinti zao kwenda shule na kuwaozesha, kwa mbadala wa mifugo.

Ikitajwa mzizi wa mazungumzo hayo ni kwenye vulabu vya pombe, wazazi huwatisha wengi hasa watoto wao kutofanya vema kwenye mitihani yao ya mwisho, hasa darasa la saba na kidato cha nne, ili wanapofeli huwaozesha katika umri mdogo, pia vifo vitokanavyo na uzazi.

Baadhi ya wazazi huwapeleka watoto wao kwa waganga wa jadi wawapo masomoni, wakiwaogesha dawa za mvuto wa mapenzi na waganga hao wanaichukulia hiyo kuwa sehemu ya kujipatia fedha na mali kama ng'ombe kutoka kwa wazazi.

Sasa hali iliyoko katika kata za Shilela na Bugarama, katika Halmashauri ya Msalala, kukiwapo mabinti vijana waliojifungua wakiwa na umri chini ya miaka 18 katika Kata za Shilela na Bugarama.

Halmashauri ya Msalala, sasa ambao wamepaza sauti zao na kuomba wazazi na walezi wanaowalazimisha watoto wao kutokwenda shule wachukuliwe hatua.

Mashiriki ya UN-FPA, UN-Women, Kiwohede, TAHA, pamoja na TGNP, kwa sasa yanatekeleza

mradi wa miaka mitatu na kuwawezesha wasichana na wanawake wapinge ukatili wa kijinsia katika Wilaya ya Ikungi mkoani Singida na Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga.

**MABINTI SHILELA/BUGARAMA**

Veronica Muhalale (19), mkazi wa kijiji cha Marito Kata ya Shilela katika Halmashauri ya Msalala, anasema wazazi ni chanzo cha mabinti kukatisha masomo yao, kwa kuwalazimisha kuacha masomo na kuolewa katika umri mdogo, kwa mbadala wa kupata ng'ombe, mjadala ukifanyika vilabuni.

Anasema, imefikia hatua wazazi wanawatisha mabinti wafanye vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho darasa la saba na kidato cha nne na wanapofeli, hulazimishwa kuolewa, wazazi wakilenga kupataa fedha na ng'ombe na mlegwa anapokataa, familia hukumbana na visa vya kifamilia, mabinti wakihangaika vijijini bila ya msaada.

"Mimi baba yangu alinizuia kwenda shuleni, niliacha shule nikiwa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Nyikoboko mwaka 2019. Nilikuwa nafanya vizuri kwenye masomo yangu, mwanaume aliyetaka kunioa wakati huo alinipatia mimba na kutoweka... mpaka sasa mtoto ana miaka miwili sijawahi kumwona," anasimulia.

Muhalale anaendelea: "Siyo mimi niliyofanyiwa haya, wapo wengi ila sema wanaogopa kupaza sauti kwa kuhofia wazazi wao kuchukuliwa hatua, serikali kwa kushirikiana na mashirika yanayotetea haki za wanawake na mabinti wafike vijijini ambako haya yanatendeka."

**VIKUNDI UJASIRIAMALI**

Halima Ramadhani, kutoka Kata ya Bugarama anasema alijifungua mtoto katika umri wa miaka 17 na sasa ameshapata elimu ya uzazi wa mpango, inayomsaidia kudhibiti mimba tena akiwa na mtoto mdogo, lengo ni kuhakikisha ndoto zake kwa kujihusisha na ufundi cherehani aliyowezeshwa na Asasi ya Kiwohende.

Halima Ramadhani, Mwenyekiti wa Kikundi cha Mabingwa Klabu kata ya Bugarama chenye wasichana 78 wahitimu wa mafunzo ya ushonaji, umeme, huduma za steshenari na udereva.

Anasema, alilazimika kumuacha mtoto nyumbani kwake akiwa na miezi sita na kuhudhuria mafunzo hayo katika Chuo cha Mwakata kupitia ufadhili wa Kiwohede.

"Tumetoka chuoni, tumepata vitu tofauti na sasa kila msichana amejiwezesha kiuchumi na wengine wameajiriwa. Sisi mafundi cherehani tunaomba kupatiwa tenda za ushonaji wa sare za shule kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kata hii," anaeleza Ramadhani.

Veronica Charles, ana maoni kuwa, baada ya kuhitimu mafunzo hayo alipambana kwa kukodi cherehani na sasa ameweka malengo ya kununua ya kwake, akilega awe mfano katika eneo lake kwa kufanya vizuri na kubadilisha mtazamo wa jamii juu ya watoto wa kike.

"Tumejifunza ujasiriamali, tunashona nguo na kikundi chetu kina wasichana 11 waliozalishwa katika umri mdogo. Kwa sasa tunajiamini na mafunzo haya yamenisaidia katika maisha yetu.

"Tunalea watoto wetu bila ya kuwategemea wazazi. Wito wetu, wazazi wahamasishwe kutowakatisha tamaa watoto wao na kuwaachisha masomo," anasema Veronica.

Mwingine ni Revina Paul, anasema baada ya mafunzo hayo ya ufundi, sasa hawadharauliki tena kifamilia, wanaheshimika na kutoa msaada unaowainua kiuchumi kifamilia, wakiwa katika uwezo sawa na wanaume.

**OFISA MAENDELEO YA JAMII**

Erasto Ching'oro, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Jinsia, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, anautaka uongozi wa mkoa Shinyanga kushirikiana na Halmashauri ya Msalala kuweka utaratibu mzuri utakaovisaidia vikundi hivyo na kuvirasimisha.

Anasema, mabinti hao wanapaswa kusajiliwa kama vikundi na kunufaika na asilimia nne zinazotolewa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani, hivyo maofisa maendeleo ya jamii waliweke hatua hiyo utaratibu mzuri utakaowasaidia kuwainua kiuchumi zaidi. Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, ambaye ni Mratibu wa Mkoa wa Kamati ya Mtakuwwa, aliwaagiza maofisa maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii katika halmashauri hiyo kuhakikisha vikundi hivyo vinasajiliwa hadi kufikia taerehe 30, mwezi uliopita.

Ngwale anamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Simon Berege, anaweka jitihada za kutambua vikundi vya mabinti waliojifungua katika umri mdogo wanajishughulisha na waingizwe kwenye utaratibu wa kupata mikopo.

**MASHIRIKA WATETEZI**

Justa Mwaituka, Mkurugenzi wa Shirika la Kiwohede, linalovisimamia vikundi hivyo kupata mafunzo ya stadi za maisha, anasema walishafanya mchakato wa utambuzi kwa wasichana hao na wengine waliokuwa wameolewa, nao waliwapa fursa ya kunufaika na mafunzo hayo.

Anasema, katika kata ya Shilela walihitaji wasichana 75 kuwapa maarifa na stadi za kazi, wakihudhuria vipindi vya radio, ili kuwapa uzoefu wenzao katika madhira waliyoyapitia, ikiwamo kukatisha masomo na kuolewa katika umri mdogo.

"Wamepata mafunzo ambayo tayari tumeanza kuona kazi zao na tunahitaji kuendelea kuwatia moyo ili wazidi kujiamini zaidi na kazi zao," anasema Mwaituka.

Mratibu wa Kutokomeza Ukatili Kijinsia dhidi ya Wanawake na Watoto UN Women -Tanzania, Lucy Tesha, anayehimiza umuhimu wa kuendelea kuelimisha jamii izikabili changamoto zinazowakabili wasichana, kwani kutowashirikisha kwenye fursa za kiuchumi kifamilia inarudisha nyuma pato la Taifa.

Mwakilishi wa Shirika la UN-FPA Kanda ya Ziwa, Amir Batenga, anataka jukumu lao ni kuwaelimisha wazazi kutambua haki ya mtoto kwenda shule na mradi unalenga kila mtoto anayepaswa kwenda shule, afike huko kutimiza ndoto zake na muhimu kuwa mbali na kuwaozesha mapema.

Anaomba Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii, iwatembelee kila mara maeneo yenye mradi na kuhakikisha watoto wanakwenda shule.

**KAMATI YAUNDWA**

Katibu Msaidizi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kijiji cha Malito Kata ya Shilela, Joseph Mbunge anasema wamekuwa wakiwahamasisha wazazi wawapeleke watoto shule na kupunguza utoro. Wanafunzi 127 walifuatiliwa na kurejeshwa shuleni, kuendelea na masomo.

Malalamikio yake ni kuibuka matukio ya mimba na ndoa za utotoni wanayoyaripoti kwenye mamlaka husika, kukiwapo kesi mbili za mimba kwa mwanafunzi wa darasa la tano na kidato cha tatu zinazoendelea.

Anasema, kukosekana hosteli ya wasichana katika Shule ya Sekondari Nyikoboko, inachangia mimba nyingi, akilaumu wazazi kutengana kunasababisha mabinti kubebeshwa majukumu mazito ya kifamilia na inawapotezea umuhimu wa elimu.

Nyakwesi Gunya, anayetoka kata ya Lunguya, anasema, wamekuwa wakitumia mikutano ya hadhara kukielimisha jamii na wanapokea taarifa za matukio ya ukatili wanayoyafanyia kazi.





# RC aonya viongozi kuwa kikwazo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewaagiza viongozi wa serikali kuanzia ngazi za chini kutokuwa kikwazo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo bali wawe sehemu ya kuwawezesha kukua ili kufikia malengo.

Mtaka aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara wadogo wadogo jijini hapa ili kusikiliza kero zinazowakabili katika biashara.

Alisema viongozi wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuwaongoza wafanyabiashara ili wapige hatua na kufuata kanuni zinazotakiwa katika ufanyaji biashara.

"Naomba viongozi muwe sehemu ya kuwasaidia hawa. Na nyie wafanyabiashara zingatieni sheria na kanuni za kufanya biashara ili msilete athari kwa wananchi wengine wakati wa kutimiza majukumuyenu," alisema Mtaka.

Wakifanya hivyo, alisema ana hakika kutakuwa hakuna ushindani wowote kati yao na viongozi wa mamlaka pale wanapotekeleza majukumuyao.

Mtaka pia aliwaruhusu wajasiriamali wa Jiji la Dodoma kufanya biashara zao hadi usiku huku akiahidi kuwaboreshea miundombinu ili kuendesha shughuli zao bila bugudha yoyote.

Alisema serikali ya mkoa itashughulikia tatizo la ukosefu wa taa za barabarani pamoja na kuhakikisha ulinzi unakuwapo muda wote.

Kuhusu eneo la Nyerere Square ambalo wanafanyia biashara, alisema hawawezi kuwaongezea muda kama walivyotaka huku akiwataka kutii sheria ya kutopanga bidhaa asubuhi katika eneo hilo kwa sababu ni barabara.

Alisema wanatakiwa kutimiza masharti yaliyowekwa ili kufanya biashara zao kihalali bila kukimbizana na mgambo wa jiji.

Katika mkutano huo, wafanyabiashara wadogo waliomba serikali iwapange katika maeneo na kuyarasimisha ili wasipate bugudha kutoka kwa askari na mgambo wa jiji.

Akizunguza kwa niaba ya wenzake mfanyabiashara, Hamisi Juma, alisema serikali inapaswa iliangalie suala la kuwapa maeneo ili kufanya biashara zao bila bugudha yoyote.

"Tunaomba serikali iliangalie hilo kwa sababu tukianza kukimbizana na askari na mgambo wa jiji tutashindwa kufanya biashara kwa ufanisi na badala yake tutaingia hasara," alisema Juma.

## Wenye ulemavu waomba msaada

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATOTO wenye ulemavu wa ukoma katika makazi ya Msamaria, Hombolo jijini Dodoma, wameomba kuwezeshwa fedha na serikali pamoja na wahisani ili kuanzisha miradi itayawasaidia kuwakwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Asasi ya Mfuko wa Mtoto wa Shule kutoka Familia za Ukoma (LFSC), Philemon Ulanga, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kwa niaba ya watoto wanaoishi kwenye makazi hayo.

Ulanga alisema kuwa ili kujikwamua kwenye maisha hayo duni kwa watu hao wenye ulemavu wa ukoma na kujiimarisha kiuchumi, serikali, taasisi za kidini mashirika na watu binafsi wanaombwa kuwawezesha.

"Makazi ya wazee wenye ulemavu wa ukoma wataendelea kuombaomba kutoka kwa wasamalia wema mpaka lini? Ifike wakati sasa vijana na mabinti wanaoishi na wazazi wao hao, wawezeshwe kifedha ili waendeshe miradi endelevu itakayowaondoa kwenye hali ya kuombaomba," alisema.

Aidha, Mkurugenzi huyo ameiomba jamii kuondokana na mtizamo hasi wa kuona kuwa ugonjwa huo ni laana na mikosi, bali kinachotakiwa ni kuangalia ni jinsi gani wanavyoweza kuwasaidiwa ili kujisimamia.

"Bado kuna dhana potofu kwa baadhi ya jamii ambayo imekuwa ikiogopa hata kukaa karibu nao kwa kufikiri kuwa wataambukizwa suala ambalo linaloonyesha wazi kuwa bado kunatakiwa elimu ya kutosha kwa jamii ili waondokane na tabia ya ubaguzi na unyanyapaa," alisema.

Mwasisi wa Asasi ya Raymond Foundation Account (RAFOA), Mwalimu Raymond Mapuli, aliwaomba Watanzania kuelekeza upendo wao kwa watu wenye ulemavu wa ukoma kuwasaidia matibabu, chakula na mavazi.

Alisema watu wenye ulemavu wa ukoma wamesahaulika kisera na kujikuta wako katika mateso kwenye maisha yao kutokana na kukosa mahitaji muhimu.



Wananchi wakiangalia mabaki ya vibanda vilivyoungua moto katika Barabara ya Tabora, jijini Dodoma juzi usiku na kuteketeza mali za wafanyabiashara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wanahabari wapewa neno magonjwa yasiyoambukiza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VYOMBO vya habari vimetakiwa kutumika kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya magonjwa yasiyoambukiza ili kusaidia kuyadhibiti.

Mtafiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Dk. Emmanuel Makundi, alisema juzi katika warsha ya wanahabari na watafiti kutoka sekta mbalimbali jijini Dodoma ilioandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Dk. Makundi alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika usambazaji wa elimu ya magonjwa hayo kutokana na kutoa taarifa sahihi zinazotolewa na watafiti au wataalamu wa sekta mbalimbali juu ya magonjwa hayo. Alisema mchanganuo wa kupambana na magonjwa haya unaonyesha kwa mwaka Sh. milioni 702.9 zinahitajika sawa na asilimia 35.6 ya matumizi ya sekta ya afya.

"Tunaomba vyombo vya habari viwe mstari wa mbele katika kusambaza taarifa kuhusu elimu ya kuzuia magonjwa yasioambukiza kwa sababutaarifa huwafikia kwa urahisi wananchi," alisema Dk. Makundi.

Alisema utafiti zaidi unahitajika kwa kuwa magonjwa hayo nchini hayajulikani, ili kuziba pengo la maarifa kwa kuwa wengi wao hawajui juu ya magonjwa hayo.

Pia alisema kunahitajika kuundwa kwa kamati inayojumuisha sekta zote muhimu ambayo itasaidia kuratibu mapambano kuhusu kinga nakudhibiti tatizo hilo.

Mbali na hilo, alisema kunapaswa kuimarishwa kanuni na kuhimiza utekelezaji wa sheria na kanuni zinazohusiana na mapambano dhidi ya magonjwa hayo, ikiwamo umuhimu wa kutekeleza mambo muhimu yaliyoko katika mwongozo.

Alisema utafiti zaidi unahitajika kwa magonjwa hayo, hivyo ni vyema jamii ikapata elimu inayotolewa na watafiti kupitia vyombo vya habari.

Mkurugenzi wa Menejimenti ya Maarifa wa COSTECH, Dk. Philbeth Luhunga, alisema vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa katika utoaji taarifa mbalimbali za utafiti zinazofanywa na watafiti.

Alisema hivi sasa jamii imekuwa mstari wa mbele katika utumiaji wa teknolojia ya TEHAMA, hivyo ni rahisi kupata taarifa kupitia vyombo vya habari.

Kutokana na hilo alisema COSTECH imekuwa mstari wa mbele kuwashirikisha wanahabari pamoja na watafiti katika kuzungumzia mambo mbalimbali yanayogusa jamii kiafya, kiuchumi na maendeleo.

Alisema warsha hiyo ina umuhimu mkubwa sana kwa sababu inawasaidia wanahabari kupata habari sahihi kutoka kwa watafiti nao huzitoa kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali.



# Waziri atoa mwezi mkandarasi maji kulipwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Marryprisca Mahundi, ametoa mwezi mmoja kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kumlipa mkandarasi anayejenga mradi mkubwa wa maji uliopo Mamlaka ya Mji wa Makongolosi wilayani Chunya.

Mhandisi Mahundi alitoa maagizo hayo juzi alipotembea na kukagua mradi huo akiambatana na viongozi mbalimbali wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) pamoja na watendaji wa Mamlaka hiyo.

Alisema mradi huo unatumia kiasi cha fedha shilingi bilioni mbili na milioni 800 hadi kukamilika kwake na kwamba hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 270 kinadaiwa na mkandarasi huo.

"Nimefurahishwa na kazi ya ujenzi wa mradi huu bila kujali unaidai serikali wakati mwingine unatumia gharama zako ili kazi isikwame tunapenda makandarasi wenye moyo wa kizalendo kama wewe nakuahidi hela yako utapata na nakuhakikishia tumekuamini tutaendelea kushirikiana na wewe kwenye miradi mingine. Hadi sasa mradi huo umekamilika kwa asilimia 90," alisema Mhandisi Mahundi.

Mkandarasi wa kampuni ya Make Engineering ambaye anayejenga mradi huo, Tanda John, alisema mradi huo utamilika ndani ya muda uliopangwa kwa mujibu wa mkataba.

Alisema atahakikisha mradi huo unakamilika mapema ili wakazi wa Makongolosi na Matundasi wilayani Chunya waanze kunufaika na majisafi ya bomba.

Aliishukuru serikali kwa kuahidi kumlipa kiasi cha fedha shilingi 270 na kuahidi mradi huo utakuwa wa mfano nchini.

Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Gilbert Kayange, alisema wataendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya maji ili wananchi wafurahie huduma ya maji ya bomba.

Aidha, aliwasisitiza wananchi kuendelea kulipa bili za maji ili Mamlaka hiyo iendelee kujenga miradi mingine ya maji katika maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliwaomba wananchi kuacha tabia ya kuharibu miundombinu ya maji, na kwamba yeyote atakayebainì hatua kali za kisheria zitachukuliwa alisisitiza jamii ya wafugaji kutopasua mabomba ya maji kwa ajili ya kunywesha mifugo yao.



Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hans Patrick (wa pili kulia), akipokea maelekezo kutoka kwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (katikati), alipotembelea chanzo cha maji cha Makongolosi kwenda kwa wakazi wa maeneo mbalimbali ya wilayani Chunya, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Sababu TARI kuinua kilimo cha ufuta hizi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), imeanza mikakati ya kuinua kilimo cha ufuta, lengo kukabiliana na uhaba wa mafuta ya kupikia unaolikabili taifa kwa sasa.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema mbali na kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta nchini, pia lengo la serikali ni kuongeza tija kwenye kilimo cha zao hilo ili kuinua kipato cha mkulima na serikali kwa kuongeza uzalishaji utakaoongeza mauzo ya zao hilo.

Vilevile, alisema serikali inalenga kuboresha lishe kwa wananchi ili kukabiliana na tatizo la udumavu linaloikumba mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo inazalisha chakula kwa wingi, lakini bado tatizo hilo lipo juu kuliko kiwango cha kitaifa.

"Tunataka kuongeza tija kwa maana ya kwamba katika eneo lako dogo ulilonalo mkulima utumie mbinu za kisasa kuzalisha, utumie mbegu bora ambazo zimefanyiwa utafiti ili upate mazao mengi, kwa sasa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa mafuta, sasa hii ni fursa kwetu wakulima wa karanga," alisema Nzunda. Aliwataka wananchi kutumia fursa ya uwapo wa watafiti hao kujifunza mbinu bora za kilimo ili waachane na kilimo cha mazoea ambacho huwa kinawapatia mazao ya kujikimu badala ya kuzalisha kibiashara.

Alisema tayari ugunduzi wa mbegu bora za ufuta umeshafanyika kwa kuzingatia mazingira mbalimbali ya nchi kulingana na hali ya hewa na uwezo wa kuhimili visumbufu. "Hizi mbegu ni nzuri kwa sababu zinahimili magonjwa na visumbufu vingine vya mimea, hivyo tunawashauri wakulima waachane na mbegu za kienyeji ambazo wamekuwa wakizitumia na watumie mbegu hizi bora ili waongeze tija," alisema Dk. Bucheyeki.

Nao baadhi ya wakulima kutoka kata za Simambwe na Ijombe waliiomba serikali iwasaidie kupata mbegu kwa wakati na kuwasaidia upatikanaji wa masoko ya uhakika ya zao hilo.

# Kinamama walaumiwa utapiamlo wa watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

BAADHI ya wanawake mkoani Mbeya, wanadaiwa kuchangia tatizo la utapiamlo kwa watoto, kutokana na kushindwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya kuhusu namna ya kunyonyesha.

Hayo yalisemwa na Ofisa Lishe wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Charles Msigwa, kwa kueleza kuwa mtoto asiponyonyeshwa maziwa ya mama kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo, ana hatari kubwa ya kukosa virutubisho muhimu, ambavyo vinahitajika kwa ajili ya ukuaji wake hivyo kusababisha utapiamlo.

Alisema baadhi ya watoto wanaopimwa kliniki katika hospitali hiyo, afya zao sio za kuridhisha, kutokana na wengine kudhoofu na wengine kuwa na tumbo kubwa.

Alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha utapiamlo kwa watoto ni kinamama walio wengi kuwa na shughuli mbalimbali za uzalishaji na ujasirimali, hivyo hushindwa kumaliza miezi sita wakihofia kukwamisha kazi zao.

"Mtoto asiponyonyeshwa kwa miezi sita ya mwanzo anaweza kupata ugonjwa wa kwashakoo au utapiamlo, tumejitahidi kutoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama, lakini wengine hawazingatii, matokeo yake watoto wanapata maradhi," alisema Msigwa.

Aidha, Dk. Msigwa alisema zipo athari zitokanazo na mama kutomnyonyesha mtoto ikiwamo saratani ya matiti kwa sababu maziwa yanayotakiwa kutoka yanagandia ndani na kutengeneza mafuta.

Mmoja wa wanawake kutoka Mtaa wa Juhudi jijini humo, Jenifer Kabuka, alisema kinachosababisha kuwaachisha maziwa watoto ni hali ngumu ya maisha, hivyo hulazimika kwenda mashambani au kufanya shughuli za ujasiriamali ili kupata fedha za kuendesha maisha.

Jenifer alisema kwa sababu ya kuwa na shughuli nyingi za kujiingizia kipato, watoto hunyonyeshwa uji, ambao humfanya mtoto kuacha kusumbua.



# Mwinyi achukizwa matumizi fedha mabaraza miji Kaskazini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hajaridhidhwa na matumizi ya fedha kwa Mabaraza ya Miji ya Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Dk. Mwinyi amesema hayo katika mkutano wa Majumuisho uliofanyika Ukumbi wa Shule ya Bumbwini, baada ya kukamilisha ziara yake ya siku mbili katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuangalia shughuli za maendeleo.

Alisema fedha nyingi zinazokusanywa na halmashauri hizo zinatumiwa kwa matumizi yao binafsi na siyo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kutaka hilo likomeshwe.

Alieleza kuwa fedha zilizokusanywa kwa mabaraza ya mji Mkoa wa Kaskazini Unguja ni Sh. bilioni 2.45 na Kaskazini A imekusanya Sh. milioni 771 na matumizi ya miradi ya maendeleo Sh. milioni 9.4 nyingine zimetumiwa kwa matumizi ya kawaida jambo ambalo hajafurahishwa nalo.

"Fedha nyingi zinazokusanywa na Halmashauri na Mabaraza ya Manispaa zetu mnazitumia nyinyi wenyewe na sio kwa miradi ya maendeleo hili sasa liwe mwisho tulikomeshe," alisema.

"Serikali imeondoa ugatuzi kwa sekta ya afya, elimu na kilimo nyinyi mabaraza ya mji mmebaki na masuala ya usafi, kujenga masoko, vituo vya mabasi na kuwasaidia wajasiriamali mtajengaje kwa shilingi milioni tisa wakati mnakusanya milioni 700 huu ni walakini mkubwa, sasa haya yanapaswa kuchukuliwa hatua," alisema.

Kadhalika miongoni mwa hatua atakazozichukua ni kuwatumbua wakurugenzi wa mabaraza na halmashauri na kuchagua wakurugenzi wapya ili kuokoa fedha za serikali.

Alisema kuna vyanzo vingi vya mapato, lakini fedha zinapotea na zinaingia mifukoni mwa watu.

Aidha, alisema pamoja na Zanzibar kuwa nchi ya kisiwa na kuwa na wavuvi wengi, bado wanafanya shughuli zao kwa kutumia vifaa duni pamoja na kukosa masoko ya kuuzia samaki.

Alisema hatua hiyo inatokana na serikali kushindwa kuwawezesha wavuvi hao kwa kuwapatia boti kubwa na za kisasa zitakazowawezesha kufika mbali na kupata samaki wengi.

Aliiagiza Wizara ya Uchumi wa Bluu kujipanga vyema ili kufahamu idadi ya wavuvi, mahitaji yao na misaada wanayohitaji ili kusaidiwa kupatiwa vyombo vya kisasa pamoja na masoko kwa kuzihamasisha kampuni kubwa kuja nchini kuwekeza kwenye viwanda vya kusarifu samaki.

Katika hatua nyingine akiwa katika ziara yake kwenye mkoa huo, Rais Dk. Mwinyi, ameahidi kuchangia Sh. 50,000,000, kusaidia ujenzi wa Msikiti wa Jumuiya ya Fissabilillah Tabligh Markaz, uliopo Kidoti mkoni humo.

Dk. Mwinyi alitoa ahadi hiyo wakati alipoukagua na kuweka jiwe la msingi msikiti huo unaotumika kwa shughuli za Ijitmai ambao unaendelea kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema katika kuunga mkono juhudi za kuendeleza ujenzi wa msikiti huo, atachangia kiwango hicho cha fedha pamoja na kutafuta wafadhili mbalimbali, ili kusaidia maendeleo ya ujenzi wa msikiti huo mkubwa Zanzibar na kutumika ipasavyo wakati wa Ijitmai utakapofika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamaed Mahamoud, alisema ujio wa Rais Dk. Mwinyi wa kuweka jiwe la msingi katika msikiti huo utakaokuwa na uwezo wa kuswaliwa na waumini wapatao 5,500, unaonyesha imani na nia njema ya kiongozi huyo kwa wananchi wake.

Kwa upande wake, Katibu wa Mufti wa Zanzibar Shekhe Khalid Ali Mfaume, alisisitiza umuhimu wa Waislamu kutoa sehemu ya sadaka zao ikiwamo fedha, vifaa au nguvu zao katika kuendeleza mbele uislamu.

Akizungumza na wafanyabiashara wadogo, Dk. Mwinyi alisema serikali ina azma ya kuwajengea mazingira mazuri wafanyabiashara kwa kuwajengea masoko, kuwapa vitambulisho, kupunguza kiwango cha ushuru pamoja na kuwapa mitaji.

Kwa upande wao wafanyabiashara hao wadogo wakiwamo mama lishe na waendesha bodaboda, waliiomba serikali kuwajengea mazingira mazuri ya biashara zao, kupunguza ushuru na kuwapatia mitaji.

# Falme za Kiarabu kuimarisha sekta ya afya Zenji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amepokea ugeni kutoka Falme za Kiarabu wenye lengo la kuisaidia sekta ya afya katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha sekta hiyo.

Waziri Mazrui alisema ugeni huo umeahidi kukiimarisha kitengo cha usafishaji damu kwa wagonjwa wa maradhi ya figo pamoja na kujenga kituo kingine kama hicho kisiwani Pemba.

Aliyasema hayo wakati ugeni huo ulitembelea Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja na kukagua vitengo mbalimbali vilivyomo katika hospitali hiyo na kuona changamoto zilizomo. Alisema kitengo usafishaji damu kwa wagonjwa wa maradhi ya figo kina mahitaji muhimu ambayo yana gharama kubwa na ugeni huo uko tayari kukisaidia kitengo hicho kwa kukipatia mafunzo madaktari pamoja na vifaa tiba.

"Katika ziara hii nimejionea changamoto mbalimbali zinazoikabili hospitali hii hivyo naahidi pia kuzifanyia kazi na kutafuta wafadhili kusaidia ikiwamo wodi ya wazazi, chumba cha upasuaji wa maradhi ya mifupa," alisema.

Kwa upande wake Ahmad Al-falasi mwakilishi wa Al-falasi Foundation kutoka Dubai, alisema yuko tayari kuisaidia Zanzibar katika sekta ya afya na kuweka vifaa vipya pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi hao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Msafiri Marijani, alisema ujio huo utaleta faraja kubwa katika upanuzi wa hospitali hiyo kutokana na majengo yake kuwa ya zamani na kusababisha kukosekana kwa baadhi ya huduma kufanyika kwa ufanisi zaidi.




Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili Zanzibar, Dk. Soud Nahoda, akizungumza katika kongamano la mfumo wa chakula lililofanyika Maruhubi, Mjini Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mfuko maalum kuundwa kusaidia upimaji corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar imetakiwa kuunda mfuko maalum wa fedha zinazopatikana kwa upimaji corona ili kusaidia kutoa huduma bora za afya mjini na vijijini.

Hayo yalielezwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi huko Bumbwini Wilayaya Kaskazini 'B' Unguja baada ya kukamilisha ziara yake ya kikazi ya siku mbili ya kutembelea miradi ya kimaendeleo na kuzungumza na wananchi wa mkoa huo.

Alisema huduma za afya zinazotolewa katika mkoa huo haziridhishi na kuitaka wizara hiyo, kupanga utaratibu maalum kwa fedha zinazotokana na upimaji wa Covid-19 kwa kuimarisha huduma za afya ikiwamo matengenezo ya vituo vya afya, nyumba za madaktari na ununuzi wa vifaa vya hospitali.

Alisema uwapo wa mfuko huo hakutakua na ujanja wa fedha hizo kupotea na badala yake zitasaidia kuboresha huduma za afya.

"Nimejionea mimi mwenyewe changamoto zinazoikabili sekta ya afya, vituo vya afya havikidhi, sehemu nyingine vituo vya afya vipo, lakini havitoi huduma na vinavyotoa huduma bado huduma ni duni," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema ipo haja ya kuangalia namna ya kufanya ili kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa huduma za afya ikiwamo kuboresha miundombinu, dawa, vifaa tiba na kuongeza watumishi wa afya.

Aliitaka Wizara ya Afya kuangalia utaratibu wa kutengeneza mapato ya ziada nje ya utaratibu wa bajeti ili kutoa huduma bora zaidi na kujenga vituo vitakavyokidhi haja.

Akizungumzia sekta ya elimu, Dk. Mwinyi alisema katika ziara yake hiyo ameshuhudia mrundikano wa wanafunzi madarasani shuleni na kuitaka Wizara ya Elimu kuhakikisha darasa moja lisizidi wanafunzi 45 na kuboresha miundombinu ya elimu.

Alisema kuna uhaba wa walimu wa sayansi na hesabati, maslahi duni ya walimu na baadhi ya walimu wanalazimika kutoa nauli mifukoni mwao na waliopo hawaendani na fani zinazotakiwa, wizara kujipanga kuboresha maslahi ya walimu ili kuwa na elimu bora.

# Machinga waonywa biashara za barabarani

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limewataka wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, kuacha kufanya biashara ndani ya barabara.

Mratibu wa Polisi Makao Makuu Kikosi cha Usalama Barabarani, Mosi Ndozero, alisema juzi mkoani Dar es Salaam kuwa machinga wamekuwa wakihatarisha maisha yao kwa kufanya biashara barabarani.

Alisema wamekuwa wakiwaelimisha haki, wajibu na madhara ya kufanya biashara hizo kwenye mazingira hayo.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara hao kufanya baishara hizo mbali na barabara na siyo kuingia barabarani.

Mfanyabiashara wa maua, Matokeo Masoud, anayefanya biashara zake kwenye Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, anasema anakutana na vikwazo vingi ikiwa ni pamoja na wizi wa maua na ajali za barabarani.

Hata hivyo, alisema kwa sasa ajali zimepungua kulinganishwa na kipindi cha nyuma.

Hamisi Haji, dereva anayeitumia barabara hiyo alikiri kushuhudia mara kwa mara machinga wakiingia barabarani kufanya biashara, hasa kunapokuwa na msongamano wa magari.

Alisema anachokifanya kwa ajili ya usalama wake na machinga hao ni kupiga honi na kupunguza mwendo ili kuepusha ajali.

Vivian Mahenge, mkazi wa Mikocheni A wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam, alisema wauzaji wa maua wanamwathiri kwa sababu eneo la watembea kwa miguu limebanwa na bidhaa zao, hivyo hulazimika kutembelea akipita ndani ya njia ya magari.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu Hali ya Usalama Barabarani ya mwaka 2018, inabainisha kuwa takriban watu milioni 1.35 hufariki dunia kila mwaka kutokana na ajali za barabarani, huku zaidi ya nusu ya vifo hivyo vikitokana na watembea kwa miguu na ajali za pikipiki.

WHO inabainisha katika ripoti yake hiyo kuwa chanzo cha vifo hivyo ni pamoja na uzembe wa madereva, watembee kwa miguu na kukosekana kwa maeneo ya watembea kwa miguu na waendesha baiskeli.

*Imeandaliwa na Aisha Mbuma, Magreth Tweve, Goodluck Minja, Maira Levi, Bartalomew Prosper na Mziray Kiraghinja, SJMC



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (kulia), akipata maelezo kwa Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda (kushoto), alipofanya ziara katika Kiwanda cha Lodhia Group of Companies, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani hivi karibuni, ili kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kuboresha mazingira ya kazi yaliyotolewa na OSHA. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waitara asimamisha wanne TEMESA

**Na Futuna Seleman,** KIBITI

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, amewasimamisha kazi watumishi wanne wa Taasisi ya Serikali Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kutokana na usimamizi mbovu wa kivuko cha Kilindoni kinachotegemewa na wananchi wa Mafia na vitongoji vyake kuwasafirisha maeneo tofauti nchini.

Waliosimamishwa ni pamoja na Idd Saleh Sungura, Tryphon Emmanuel Kizee, Wemael Kiangi na Felician Mgeta, baadhi wakituhumiwa kuwa na lugha chafu, ubadhirifu wa fedha za serikali huku kapteni wa meli hiyo MV Kilindoni, Habib Mbarouk, akipewa onyo la kuacha kutoa majibu machafu kwa wananchi wanaotumia kivuko hicho.

Waitara alitoa uamuzi huo katika bandari ndogo ya Nyamisati, wilayani Kibindi, mkoani Pwani baada ya kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi na viongozi wa chama na serikali kuhusu usimamizi mbovu wa kivuko hicho.

"TEMESA lazima ifumuliwe kila unapogusa aibu ukienda katika karakana yao ipo kama kijiwe hii idara, ni mara yangu ya mwisho kumzungumzia DG (mkurugenzi mkuu) wa TEMESA hili nalipeleka kwa waziri kulifanyia maamuzi kwa sababu kuna mvutano wa maneno na mahusiano sio mzuri watumishi wametajwa katika mazingira haya nawasimamisha," alisema Waitara.

Hata hivyo, alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamissi kwa kuendelea kufanyia kazi mapendekezo ya wadau na maagizo ya serikali kuhusu uboreshaji wa huduma za Bandari nchini.

Akiwa katika Bandari ya Nyamisati, Naibu Waziri alitembelea eneo ambalo wafanyabiashara ndogo ndogo wanaosafirisha mizigo kutoka au kwenda Bandari ya Mafia ambao baadhi yao walitoa maoni ya kuboresha huduma za bandari hizo.

Moja kati ya mambo yaliyotajwa na wafanyabiashara hao na serikali kuahidi kufanyia kazi ni pamoja na kuona namna ya kupunguza tozo za huduma za usafirishaji wa mizigo katika bandari hizo. Wakazi wa maeneo ya Kibiti na Mafia kwa kiwango kikubwa wanategemea usafiri wa njia ya maji kusafirisha mizigo ikiwamo saruji, gesi, vyakula, vifaa vya ujenzi pamoja na bidhaa nyingine muhimu kwa mahitaji ya nyumbani.

Akizungumzia tozo za huduma ya mizigo kwa upande wa Bandari, Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Eric Hamissi, alisema tayari suala hilo limeanza kufanyiwa kazi na litapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Katika Bandari ya Nyamisati tayari TPA imetekeleza jukumu lake la msingi na la kisheria la kujenga na kuendeleza miundombinu ya Bandari ili kuziwezesha taasisi nyingine za serikali na wadau kutoa huduma. Mfano kwa kupitia miundombinu ya Bandari ni jukumu la TEMESA kutoa huduma za vivuko na meli ambazo zinazotumika kusafirisha abiria na mizigo.

Akiwa katika Bandari ya Nyamisati, Waziri Waitara aliiagiza TEMESA kufanyia kazi changamoto zilizoelekezwa kwao na wananchi maeneo ya Kibiti na Mafia ili kufikia lengo la serikali la kutatua kero ya usafirishaji katika eneo hilo lililozungukwa na bahari.

# Lukuvi awatega watumishi ardhi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema watumishi wa ardhi watakaohusika kumilikisha kiwanja kimoja mara mbili watachukuliwa hatua kali.

Aliyasema hayo jana baada ya kukagua shughuli za utendaji wa sekta ya ardhi kwenye banda la Wizara katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa maarufu Sabasaba, Dar es Salaam.

Alisema ikibainika kuna umilikishaji mara mbili uliosababishwa na watumishi, wote waliohusika kama ni ofisa upimaji, upangaji na mmilikishaji, watachukuliwa hatua.

Lukuvi alisema awali sekta ya ardhi ilikuwa na migogoro mingi, lakini tangu mwaka 2015 kero nyingi hazipo au zimepungua kwa kiasi kikubwa.

"Ni kweli huko nyuma tulikuwa na kero nyingi sana katika Sekta ya Ardhi na ninaamini tangu mwaka 2015 migogoro hakuna au imepungua sana. Nisisitize kama kuna utoaji hati mara mbili wote walioshiriki kuanzia wale wa kupima, kupanga na yule aliyemilikisha watachukuliwa hatua," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, makamishna wa ardhi wasaidizi kwenye ofisi za ardhi za mikoa wanatakiwa kuhakikisha hakuna mgogoro mipya kwenye maeneo yao na kusisitiza kuwa ni marufuku ofisi hizo kushiriki au kuchangia mgogoro wa ardhi.

Lukuvu alibainisha kuwa kwa sasa wizara yake imeanza kubadilika ambapo uandaaji na utoaji hatimiliki za ardhi umetoka kwenye mfumo wa analogia kwenda digitali na kusisitiza kuwa hayo ni mageuzi makubwa.

Kuhusu mfumo wa kidigitali, Waziri Lukuvi ambaye alikabidhi hati za kielektroniki za papo kwa hapo kwa baadhi ya wananchi waliotembea banda la wizara, alisema umeasisiwa na vijana wazalendo wa kitanzania na lengo lake ni kuzuia makosa ya kibinadamu na kuongeza kuwa anaamini migogoro inayosababishwa na tamaa za kibinadamu za watumishi itapungua.

Waziri pia alitembelea banda la Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na kusifu ubunifu wa shirika hilo katika ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha mkoani Dodoma katika maeneo ya Iyumbu na Chamwino.

Alilitaka shirika hilo kuhakikisha wananchi wanaolipa fedha kwa ajili ya kununua nyumba wanapatiwa nyumba hizo na kumilikishwa mara tu baada ya kulipa.

# Rais wa Haiti auawa, mkewe ajeruhiwa

**Port-Au-Prince,** HAITI

RAIS wa Haiti Jovenel Moise, ameuawa katika shambulio dhidi ya makazi yake mjini Port-au-Prince, amesema Kaimu Waziri Mkuu Claude Joseph

Joseph alisema makazi ya rais yaliyopo Port-au-Prince yalishambuliwa na watu wasiojulikana waliojihami kwa silaha saa 01:00 (05:00 GMT).

Mkewe, Martine Moïse aliripotiwa pia kujeruhiwa katika shambulio hilo.

Joseph alisema kuwa hatua zote zilichukuliwa ili kuhakikisha kuendelea kwa serikali na kutaja tukio hilo kitendo cha kuchukiza, kisicho cha kibinadamu.

Jovenel Moïse (53), alikuwa madarakani tangu Februari 2017, baada ya mtangulizi wake, Michel Martelly kung'atuka mamlakani.

Wakati wa Moïse ofisini, ulikuwa mgumu alipokabiliwa na tuhuma za ufisadi na alikabiliwa na mawimbi ya maandamano ya mara kwa mara ya kupinga serikali yake.

Mwaka wa 2019 wakati wa mojawapo ya maandamano kama hayo, rais huyo alisema hatoondoka nchini kwa sababu ya shinikizo kutoka kwa magenge yaliyojihami na walanguzi wa dawa za kulevya.

Kulikuwa na maandamano yaliyoenea katika mji mkuu na miji mingine mapema mwaka huu, watu wakimtaka ajiuzulu.

Upinzani nchini humo, ulisema kwamba kipindi cha miaka mitano cha Moïse kilipaswa kumalizika Februari 7, mwaka huu, miaka mitano hadi siku hiyo tangu Martelly aondoke madarakani.

Moïse, hata hivyo, alisisitiza alikuwa na mwaka mmoja zaidi wa kutumikia, hakuingia madarakani hadi Februari 7, mwaka 2017.

Kucheleweshwa kwa mwaka mzima, kulisababishwa na madai ya udanganyifu katika uchaguzi ambao mwishowe ulisababisha matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 kufutiliwa mbali na Moïse alitangazwa mshindi.

Misukosuko ya muda mrefu, udikteta na majanga ya asili yameiacha Haiti kama moja ya mataifa maskini kabisa katika eneo la Amerika.

Tetemeko la ardhi mwaka wa 2010 liliua zaidi ya watu 200,000 na kusababisha uharibifu mkubwa kwa miundombinu na uchumi.

Kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa (UN), kilitumwa mwaka 2004 kusaidia kuleta utulivu Haiti iliyo na takribani na watu milioni 11, kikosi hicho kiliondoka mwaka 2017.

Majira ya asubuhi jana kwenye maeneo tofauti na mitaa, ikiwamo Caribbean na mji mkuu Port-au-Prince, yalikuwa wazi wakihofia usalama.

**BBC/AP**




Magari ya jeshi yakiwa yameweka zuio kwenye lango la kuingilia Petion Ville, jirani na makazi ya Rais Jovenel Moise, mji mkuu Port- Au-Prince, jana. Moïse aliuawa jana akishambuliwa nyumbani kwake huku mke wake, Martine Moïse akijeruhiwa na kulazwa hospitalini. **PICHA: AP**

# Lungu atangaza rasmi siku ya kuzaliwa Kaunda kuwa kitaifa

**Lusaka,** ZAMBIA

RAIS wa Zambia, Edgar Lungu ametangaza rasmi siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa Hayati Keneth Kaunda itakuwa ni siku ya kitaifa.

Amesema siku hiyo itakuwa maalumu kumkumbuka kutokana na uwajibikaji wake.

Akizungumza na waombolezaji katika kanisa kuu, Holy Cross kulikofanyika misa ya mazishi jana, Rais Lungu alisema Kaunda aliamini katika upendo na kwamba anakumbukwa kama mazalendo.

Alisema serikali itahamasisha kauli mbiu ya 'One Zambia One Nation' huku akiwaasa familia ya Kaunda kuwa wamoja.

Pia Askofu wa Sinodi ya UCZ, Sydney Sichilima, alisema amani na upendo kwa taifa uende kwenye sanduku la kura Agosti, mwaka huu. Mtoto wa Kaunda, Panji alisema kifo cha baba yake kitumike kuhamasisha mema aliyoyatenda, kuepuka vurugu na kwamba wapinzani wawaambie wafuasi wao kuepuka vurugu.

Viongozi wengine waliohudhuria mazishi hayo ni Joachim Chissano na Rupiah Banda.

Kaunda alitarajiwa kuzikwa jioni katika makaburi wanayozikwa marais, eneo la 'Independence Avenue' huku maziko yake yakikamilisha siku 21 za maomboleza ya kitaifa. Kaunda alifariki dunia Juni 17, mwaka huu akiwa na umri wa miaka 97, aliongoza nchi tangu mwaka 1964 hadi 1991.

**ZNBC/RFI**

## Zimbabwe yatoa noti ya thamani kupindukia

**Harare,** ZIMBABWE

KUANZIA jana, Zimbabwe itaanza kusambaza noti mpya ya dola 50, ikiwa ndio yenye thamani kubwa zaidi kuwahi kutolewa Zimbabwe tangu mwaka 2019.

Dola 50 ya Zimbabwe ina thamani ya dola ya Marekani 0.60.

Noti mpya ilizunduliwa juzi na Benki Kuu ilisema kuwa itasambaza dola milioni 360 za Zimbabwe kupitia benki.

Imetolewa huku nchi hiyo ikikabiliwa na mfumuko wa bei ambao umewafanya watu kutembea lundo la noti.

Noti mpya ina picha ya shujaa wa kupambana na ukoloni Mbuya Nehanda.

**BBC**

## Mzozo watokota iwapo Zuma akamatwe

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

ALIYEKUWA Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, anajadiliwa iwapo akamatwe au la, kulingana na hukumu ya wiki iliyopita ya Mahakama ya Katiba kwa sababu alipatikana na hatia ya kutoheshimu agizo la mahakama.

Haijafahamika wazi, hata hivyo ni nini kitakachotokea kwake.

Msemaji wa Wakfu wa Jacob Zuma, Mzwanele Manyi aliiambia BBC kuwa haamini kwamba Zuma atakamatwa.

"Kulingana na sisi hakuna kukamatwa kutakakotokea kwasababu mtu wa kumkamata amerekodiwa akisema anasubiri mchakato ukamilike," alisema.

Manyi alisema kuwa Waziri Bheki Cele aliiandikia mahakama akisema kuwa atasubiri mchakato utakaomwongoza katika utekelezaji wa kukamkamata.

Mawakili wa rais huyo wa zamani wamekwenda kwenye mahakama ya juu zaidi kuzuia kukamatwa kwake.

Cele pia alisema kuwa ataheshimu uamuzi wa Mahakama ya Katiba.

Profesa wa Sheria ya Katiba katika Chuo kikuu cha Cape Town, Pierre De Vos, aliiambia BBC kwamba kama muda wa mwisho wa kujisalimisha ambao ni siku ya jana, aliopewa hautaheshimiwa, atakuwa tena amefanya kitendo cha kutoheshimu agizo la mahakama na uhalali wa mfumo wa sheria utakuwa umetishiwa.

**BBC**

## HABARI MICHEZO



# ITALIA yatangulia fainali Euro 2020

**LONDON, England**

TIMU ya Taifa ya Italia imetinga hatua ya fainali ya Euro 2020 baada ya ushindi wa penalti 4-2 dhidi ya Hispania kwenye mchezo wa nusu fainali, juzi.

Mchezo huo uliokuwa na ushindani mkubwa, ulichezwa Uwanja wa Wembley ambapo Italia walianza kupachika bao la kuongoza dakika ya 60 kupitia kwa Federico Chiesa.

Mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata aliweka usawa bao hilo la awali la Italia dakika ya 80 na kufanya dakika 90 za awali ubao kusoma Italia 1-1 Hispania.

Sasa Italia wametinga rasmi kwenye hatua ya fainali itakayopigwa Jumapili katika Uwanja wa Wembley, ambapo inaweza kucheza na England ama Denmark kutegemea timu iliyoibuka na ushindi jana usiku.

Wakati huo huo, Kocha wa timu ya Taifa ya Hispania, Luis Enrique, amesema hana malalamiko kuhusu timu hiyo kuondolewa kwenye nusu fainali ya Euro 2020 baada ya kufungwa kwa mikwaju ya penalti na Italia, akisisitiza anawapongeza wachezaji kwa juhudi zao kwenye michuano hiyo.

Tukio la Morata kukosa penalti kulionekana muhimu wakati penalti ya Jorginho ilipowapeleka fainali 'Azzurri' hao.

"Si usiku wa huzuni kwangu, siyo kabisa. Bila shaka kuna mambo ya kukatisha tamaa, lakini huo ndio mpira wa miguu. Unapaswa kujifunza kushinda na kushindwa. Tulizungumza kwa kiasi kikubwa kuhusu namna tulivyotaka kucheza, wachezaji waliamini katika hilo na naweza tu kuwapongeza, sina malalamiko," alisema Enrique.

## Guardiola akata tamaa Man City

**MANCHESTER, England**

NI wazi Pep Guardiola amekata tamaa huku Manchester City wakiondolewa kwenye ramani ya kumpata mrithi wa Sergio Aguero msimu huu.

Man City walikuwa sokoni kutafuta mrithi wa Aguero baada ya mchezaji huyo kuondoka Man City na kutimkia Barcelona.

Miongoni mwa wengi, Harry Kane na Erling Haaland ni wachezaji wawili waliohusishwa na City.


Kwa Kane, City waliripotiwa kutoa pauni milioni 100 ili kuipata saini ya nyota huyu wa Spurs.

Pamoja na dau hilo, Spurs waliwatolea nje City wakisisitiza thamani yake ni pauni milioni 150, lakini hawana mpango wa kumuuza Kane.

Kutokana na hali ya kiuchumi iliyopo kwa sasa, Man City wamejiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho na Pep amethibitisha kuwa haoni wakisajili mshambuliaji kwa msimu ujao.

"Kwa gharama tulizopewa, hatutonunua mshambuliaji, hatuwezi kumudu. Kila timu inataabika kiuchumi, hata sisi ni hivyo. Tuna Gabriel Jesus na Ferran Torres, walifanya vizuri kwenye nafasi hii.

"Tunawachezaji wengi kwenye akademi na mara nyingi tumecheza bila namba tisa. Kuna nafasi kubwa hatutanunua mshambuliaji kwa msimu ujao."



## Bale kustaafu soka 2022

**LONDON, England**

NYOTA wa Real Madrid na timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale, anaripotiwa kwamba atastaafu soka ifikapo Juni, 2022.

Bale amerejea Madrid baada ya kumaliza msimu mmoja wa mkopo alipokuwa Spurs.

Kurejea kwa Bale Madrid ni sehemu ya kumalizia mkataba wake wa mwaka mmoja uliosalia Santiago Bernabeu.

Akiwa anapokea mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki, Bale ana mpango wa kuachana na soka pindi amalizapo mkataba wake na Madrid.

Hata hivyo, Bale bado ana nafasi ya kuipeperusha bendera ya Wales kama timu hiyo itafanikiwa kucheza Kombe la Dunia 2022.

Wales ina pointi tatu baada ya michezo miwili kwenye hatua ya makundi na ili kufuzu kucheza Kombe la Dunia, wanapaswa kumaliza kama vinara wa kundi (watafuzu moja kwa moja) au wamalize nafasi ya pili na wacheze hatua ya mtoano.

Endapo Wales watashindwa kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia 2022 Qatar, Bale ataonekana uwanjani kwa msimu mmoja pekee kabla ya mchezaji huyo kustaafu akiwa na umri wa miaka 32.



## Solskjaer kumvutia Halaand United

**LONDON, Eangland**

JINA la Erling Haaland litaendelea kutamkwa sana kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto hadi hapo klabu moja kigogo itakapofanikiwa kunasa saini yake.

Na hilo likitokea, Borussia Dortmund watakuwa wamedaka mkwanja wao mrefu kabisa.

Haaland mwenye umri wa miaka 20, tangu alipoibuka kuwa tishio akiwa Red Bull Salzburg kabla ya kutua Dortmund, amekuwa moto kwa kufunga, akipasia mipira nyavuni kama anavyotaka.

Amefunga mabao 43 katika mechi 43 alizocheza Dortmund. Alitua Dortmund, Januari 2020 na tangu wakati huo ameonyesha kuwa na njaa kali ya kufunga mabao na ndio maana dirisha hili kila kigogo Ulaya, kuanzia Real Madrid, Manchester City, Manchester United, Chelsea, Barcelona na Bayern Munich zote zinahitaji saini yake. Kinachoelezwa ni kwamba timu itakayofanikiwa kunasa saini yake mwaka huu, basi lazima itakuwa imeweka mezani mkwanja wa pauni milioni 150. Kwa mujibu wa mkataba wake, ikifika mwakani, atapatikana kwa pauni milioni 68- hivyo mwamba wa kweli ni yule atakayenasa saini yake kwenye dirisha hili la majira ya kiangazi.

Man United, Chelsea na Man City zinaongoza kwenye Ligi Kuu England kusaka saini yake, wakichuana na vigogo wengine wa Ulaya, Real Madrid, Barcelona, Juventus na Bayern Munich. Lakini Man United imehusishwa sana na straika huyo, ilishindwa kidogo tu kumnasa mwaka jana kabla ya kutimkia zake Dortmund.

Lakini, talkSPORT.com linadai kwamba kwenye orodha ya vigogo wote hao wanaosaka huduma ya Haaland, Man United ndio wenye nafasi kubwa ya kunasa saini yake na wana sababu zao kwenye hilo.

Uhusiano wa kocha Ole Gunnar Solskjaer na Haaland unatajwa kwamba ni mzuri na wawili hao wanawasiliana mara kwa mara.

Solskjaer alimnoa Haaland walipokuwa pamoja pale Molde na walikuwa na uhusiano mzuri kwelikweli na ndio maana alionekana angetua Old Trafford kabla ya kwenda Dortmund. Hata ikifika mwakani, wakati ada ya Haaland itakapokuwa pauni milioni 68, Solskjaer bado anatajwa kuwa na nafasi kubwa ya kumnasa.





# RENNES kumuuza Camavinga

**PARIS, Ufaransa**

LICHA ya Paris Saint-Germain na Real Madrid kuwa na nia ya kumsajili Eduardo Camavinga, hakuna timu yoyote kati ya hizo ambayo inatarajiwa kutoa ofa rasmi kwa mwajiri wake wa sasa, Rennes.

Kwa sasa, Manchester United wameibuka kama vinara wa kutaka kupata huduma za Camavinga msimu huu wa majira ya joto, huku 'Mashetani Wekundu' hao wakiripotiwa kuwa tayari kutoa ofa ya Euro milioni 25 kumsaini Mfaransa huyo.

Kwa mujibu wa Le Parisien, PSG haina mpango tena kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, ambaye alikuwa kinda mchanga zaidi kuifungia 'Les Blues' kwa zaidi ya miaka 70 na alishiriki kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kufuatia kujitokeza kwa Camavinga kwenye eneo la tukio, bei yake imepungua sana kutoka Euro milioni 70 ambazo Rennes walitaka kama bei ya maulizo mwaka jana.

Camavinga ameiambia klabu yake kuwa hayuko tayari kuongeza tena mkataba wake, ambao utaendelea hadi Juni 2022 na Rennes hawana nia ya kumpoteza kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa majira ya joto.

Na sasa klabu hiyo imeweka wazi kwamba ipo tayari kumuuza nyota wake huyo ili asiondoke kwa uhamisho huru.

## Mbappe aonyeshwa njia ya kushinda Ballon d'Or

**PARIS, Ufaransa**

NICOLAS Anelka amemshauri nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe aondoke klabuni hapo ili aweze kushinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia, 'Ballon d'Or'.

Anelka mwenye umri wa miaka 42, alianzia soka hapo PSG kabla ya kuondoka akiwa na umri mdogo kwenda Juventus na baadaye Arsenal.

Na sasa anaona kwamba, kama Mbappe anataka kushinda tuzo kubwa zaidi, kama Ballon d'Or, basi lazima aende kwenye ligi tofauti.

"Kama unataka sifa kubwa zaidi, italazimika kuhama kutoka PSG wakati fulani," aliiambia The Athletic.

"Chochote utakachofanya Paris kitakuwa kizuri, lakini mtu atasema kila wakati, lakini ulifanya ukiwa PSG, na si kwenye ligi bora kama England na Hispania, kwa hiyo hakushindana na wachezaji bora.

"Lazima uamue. Ikiwa unataka kushinda Ballon d'Or, ambayo ndio unapaswa kuangalia ili kufikia kiwango cha kina Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.

"Hauwezi kusema unashindana na ubora wakati wote ukiwa PSG. Ligi ya Ufaransa si rahisi, lakini si ngumu kama nyingine. Ligi ngumu zaidi iko England.

"Kwa hiyo, kama unataka kuwa mmoja wa wachezaji bora, basi fanya kile unachofanya huko Paris, lakini ukiwa na Chelsea au Manchester United ama Arsenal au Manchester City ama Liverpool.

"Au nenda Hispania kwa Madrid au Barcelona. Au labda Italia."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AIFUATA BRAZIL FAINALI COPA AMERICA

●●● Ni baada ya kuitoa kwa mbinde Colombia kwa mikwaju ya penalti kutokana na...

**BRASILIA,** Brazil

GOLIKIPA Emiliano Martinez amekuwa shujaa wa Argentina kwa kuokoa mara tatu mikwaju ya penalti dhidi ya Colombia, hivyo kuipeleka nchi yake fainali ya Copa America ambapo sasa watavaana na Brazil.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Estadio Nacional de Brasilia nchini Brazil juzi usiku, timu hizo zilitinga katika changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya mechi hiyo ya nusu fainali kumalizika kwa sare ya bao1-1 ndani ya dakika 90.

Martinez aliyejaribu kuwavuruga wachezaji wa Colombia wakati wa penalti kwa mfululizo wa maeneo yasiyokuwa na maana, alizuia mikwaju ya Davinson Sanchez, Yerry Mina na Edwin Cardona.

Lionel Messi, Leandro Paredes na Lautaro Martinez walifunga penalti za Argentina iliyoingia fainali dhidi ya nchi mwenyeji wa michuano hiyo, Brazil, itakayopigwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Maracana jijini Rio de Janeiro.

"Siwezi kusema. Walitupeleka kwenye penalti na hiyo ndio hoja ya bahati, leo ni zamu yangu kuheshimika," alisema kipa huyo wa Argentina, Martinez.

**Timu hizo zilipata nafasi kadhaa za kupata ushindi katika mechi hiyo kali iliyokwisha kwa kutokea faulu 46 na mwamuzi kutoa kadi 10 za njano.**

Kwa upande wa Brazil, yenyewe ilitangulia fainali hiyo Jumatatu kwa kuifunga Peru kwa bao 1-0.

## KWA UFUPI

**STERLING TAYARI KUSEPA CITY**
NYOTA wa Manchester City na England, Raheem Sterling yuko tayari kusikiliza ofa ya kuondoka klabuni hapo. Lakini kocha Pep Guardiola anataka winga huyo mwenye umri wa miaka 26, kubakia Etihad licha ya Real Madrid kuonyesha kumhitaji (***Athletic***).

**BALE AJIANDAA KUSTAAFU**
GARETH Bale mwenye umri wa miaka 31, anaweza kustaafu kucheza soka baada ya mkataba wake mnono na Real Madrid anaolipwa mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki utakapokoma msimu ujao. (***Mail***)

**VIEIRA AMTAKA ROGERS**
KLABU ya Crystal Palace imeanza mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Muingereza Morgan Rogers mwenye umri wa miaka 18. Kocha mpya wa klabu hiyo, Patrick Vieira anataka kuboresha na kuweka sawa uwiano wa umri katika kikosi hicho msimu huu. (***Mail***)

**PHILIPS HAONDOKI LEEDS**
KIUNGO wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 25, ana furaha kwenye klabu yake ya Leeds United na hana mpango wa kuikacha klabu hiyo ya Elland Road, kwa mujibu wa wakala wake. (***The i newspaper***)

**BARCA KUMUUZA GRIEZMANN**
BARCELONA itawapa nafasi Chelsea ya kumsajili mshambuliaji wake, Antoine Griezmann. Miamba hao wa Catalunya wanaokabiliwa na tatizo la kifedha, wanataka kumpiga bei Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 30, ili kukamilisha mkataba mpya wa Lionel Messi. (***Star***)

**UMTITI AGOMBEWA EPL**
KLABU za Manchester United na Arsenal zinataka kumsajili mlinzi wa kati wa Barcelona, Samuel Umtiti. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 27, anaonekana kutokwenda sawa na mipango ya meneja Ronald Koeman. (***Star***)

**CHELSEA, ARSENAL KWA TAPSOBA**
KLABU za Chelsea na Arsenal zinamfuatilia mlinzi wa Bayer Leverkusen na Burkina Faso, Edmond Tapsoba. Lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, amewaambia waandishi wa habari kwamba 'hakuna ofa ya uhakika na rasmi' iliyowasilishwa kwake, kwa maana hiyo ataendelea kuwa na Wajerumani hao msimu mpya utakapoanza. (***Metro***)

**SMITH AWANIWA VILLA**
ASTON Villa inaamini kwamba inaweza kumpata kiungo wa Arsenal, Emile Smith Rowe na watawasilisha dau jingine la tatu kwa ajili ya kumnasa Muingereza huyo. (***Football Insider***)

**WHITE ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL inaendelea kumshawishi mlinzi wa Brighton, Ben White mwenye umri wa miaka 23, ambapo tayari imeshawasilisha dau la pauni milioni 50 kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England. Hata hivyo, inaelezwa kwamba dau hilo halijakubalika kama inavyoripotiwa na vyombo vingi vya habari. (***Argus***)

**WILLIAM ATAKIWA SOUTHAMPTON**
KLABU ya Southampton ina uhakika wa kukamilisha uhamisho wa mkopo wa mlinzi wa Manchester United, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 20. (***Mail***)

**BURNLEY YAMFUATA HENNESSEY**
KLABU ya Burnley imeonyesha nia ya kumtaka Wayne Hennessey, aliye huru. Mlinda mlango huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 34, anatakiwa pia na klabu za Chelsea na Aston Villa baada ya kuondoka Crystal Palace mwezi uliopita kufuatia kumalizika kwa mkataba wake. (***Mail***)

## HABARI MICHEZO

# BENTEKE WA CRYSTAL PALACE ATUA TANZANIA

Na Mwandishi Wetu

IKIWA ni takribani mwezi mmoja na siku kadhaa tangu beki wa Kimataifa wa Ufaransa na Klabu ya Crystal Palace, Mamamdou Sakho kutua Tanzania na kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii, mshambuliaji wa klabu hiyo ya England, Mbelgiji Christian Benteke naye yuko nchini kwa ziara ya kitalii, imefahamika.

Sakho ambaye alitua nchini Mei mwishoni na familia yake, baada ya msimu wa Ligi Kuu England 2020/21 kumalizika, alitembelea vivutio mbalimbali vya utalii ikiwamo visiwani Zanzibar pamoja na Bunge la Tanzania, ambapo alikubali ombi la Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), la kuwa balozi wa utalii wa Tanzania.

Na katika kile kinachoonekana kama Sakho ameanza kuifanya kazi hiyo vema nafasi hiyo ya ubalozi wa utalii, mchezaji mwenzake wa Crystal Palace, Benteke, tayari ameonekana nchini akiwa viunga vya Hifadhi ya Ngorongoro.

Imeelezwa Benteke yupo nchini kwa mapumziko mafupi baada ya timu yake ya Taifa ya Ubelgiji kutolewa kwenye michuano ya Euro 2020.

Benteke alionekana akipiga picha na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) katika lango kuu la kuingia katika hifadhi hiyo.

Ujio wa mchezaji huyo mzaliwa wa Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), unakuja wakati shughuli za utalii zimeboreshwa nchini jambo ambalo linaendelea kuvutia watalii wengi nchini.

Ubelgiji ilitolewa na Italia hatua ya robo fainali ya michuano ya Euro kwa kupigwa mabao 2-1.

Benteke alikuwa miongoni mwa wachezaji waliokuwamo kwenye kikosi cha Ubelgiji kwenye michuano hiyo inayoendelea ikiwa imefika katika hatua ya fainali.




Mshambuliaji wa Ubelgiji na Klabu ya Crystal Palace ya Ligi Kuu England, Christian Benteke (kulia), baada ya kuwasili katika lango kuu la Hifadhi ya Ngorongoro. **MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yapewa mbinu kutwaa ubingwa

Na Adam Fungamwango

STRAIKA hatari wa zamani wa Yanga, Boniface Ambani, amewashauri wachezaji wa timu yake hiyo ya zamani kutodharau baadhi ya mechi, badala yake kusaka pointi tatu kwenye mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara kama inataka kutwaa ubingwa msimu ujao.

Akizungumza na mwandishi wetu juzi kutoka Kenya, Ambani raia wa nchi hiyo, aliyetamba misimu wa 2008/09 na 2009/10 akiwa na Yanga, alisema anachoona kwa miaka yote ambayo Simba inatwaa ubingwa, Yanga haiwi makini kwenye mzunguko wa kwanza, badala yake inakumbuka kuwa kuna ubingwa mzunguko wa pili wakati ligi imeshakuwa ngumu. "Yanga wajiangalie wapi wanakosea. Ligi siku zote huwa inaisha mzunguko wa kwanza. Mzunguko wa pili unaangalia tu zimebaki pointi ngapi niwe bingwa, ni wakati ambao ligi inakuwa ngumu kwa sababu kila timu inajitutumua. Zingine zinataka ubingwa, zingine zinatafuta pointi ili zibaki sehemu salama na zipo zinazojipapatua ili zisishuke," alisema Ambani ambaye alikuwa mfungaji bora msimu wa 2008/09 kwa mabao 18.

Straika huyo aliwataka wachezaji wa Yanga wasiwe na tabia ya kubagua mechi za kucheza, kukamia zingine na kudharau baadhi kwani zote zina pointi sawa.

"Tangu mwanzo wachezaji wanatakiwa washinde. Ukicheza na Mtibwa Sugar ama Mbeya City ukishinda unapata pointi tatu, siyo tu wakicheza na Simba ndiyo wanaonekana wamepania japo kweli hiyo ni 'dabi', lakini timu inayotaka ubingwa ni lazima iwe inakusanya pointi tatu kwenye michuano mingi, hasa kwenye mzunguko wa kwanza," alisema Ambani.

Aliwashauri viongozi na wachezaji kuzingatia hilo kwani wao ndivyo walivyokuwa wakifanya wakati wakicheza Yanga na kutwaa ubingwa.

Wakati akichezea Yanga, Ambani alikuwa hatari kwa kufumania nyavu, akicheza pacha pamoja na straika Mkenya mwenzake, Bernard Mwalala.

## Azam yaitafutia pumzi Simba SC

Na Saada Akida

KIKOSI cha Azam FC kitakuwa na mechi mbili za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Simba Julai 14, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema Jumatano iliyopita waliingia kambini na wachezaji wote wanaendelea vizuri na sasa wanafanyia kazi kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika mechi zilizopita ili makosa hayo yasijirudie katika mechi yao dhidi ya Simba.

Alisema wameanza maandalizi ya mechi hiyo na watakuwa na mechi mbili za kirafiki dhidi ya Pamba ya Mwanza na Jumamosi watacheza na timu nyingine.

"Hizo mechi zitatusaidia kujiweka imara na wachezaji kupata 'match fitness' kabla hatujacheza dhidi ya Simba, ambao mchezo muhimu sana kwetu kupata matokeo chanya.

"Price Dube hayuko katika mipango ya mechi hiyo kwa sababu bado hajawa fiti, hii ni miongoni mwa mechi nyingi sana kukosa, kwa mchezaji kama Dube haina maana kumkazania kucheza, anatakiwa kupewa muda na daktari afanye kazi yake na aweze kupona kabisa," alisema Vivier.

## ZBL yaanika udhaifu viongozi wa klabu

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Kuu Zanzibar (ZBL), Sheha Mohammed, amesema changamoto kubwa iliyojitokeza katika msimu uliopita wa ligi hiyo ni baadhi ya Viongozi wa Klabu kutosoma kanuni za mashindano hali iyozua mizozano pindi wahusika walipoadhibiwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sheha alishangazwa na kitendo cha viongozi wote wa klabu kushindwa kusoma kanuni ya mashindano ya msimu husika wa ligi huku baadhi yao wakishindwa kabisa kutafsiri vifungu vya kanuni pale wanapopewa adhabu.

Alisema baadhi ya viongozi hao wamejiwekea utamaduni wa kucheza ligi kimazoea licha ya kuitwa wakati wa kutoa maoni ya marekebisho ya kanuni kabla ya msimu mpya kuanza, na kufanya hivyo lakini kuzielewa na kuzitekeleza limekuwa tatizo kwao.

Sheha alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha malalamiko mengi au rufani zinazokatwa na klabu kuchangiwa na viongozi wao kushindwa kutafsiri kanuni, hivyo akawataka kuelekea msimu mpya kila klabu kuzisoma na kuzielewa ili kuondoa mizozo isiyo na tija katika maendeleo ya soka.

# Michezo

Alhamisi Julai 8, 2021

Nipashe




Benteke wa Crystal Palace atua Tanzania HABARI UK. 23

UNAPITAJE...



Beki wa Kati wa Colombia, Davinson Sanchez, akitumia nguvu ya ziada kumkaba mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi (kulia) kwenye mechi ya nusu fainali ya Copa America, iliyopigwa Uwanja wa Estadio Nacional de Brasilia, Brazil usiku wa kuamkia jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1 kabla ya Argentina kutinga fainali kwa mikwaju ya penalti 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# GOMES: NIMEISOMA YANGA

●●● Asema wamegundua walipokosea na kufanyia kazi, huku akieleza mechi za Ligi Kuu zitampa...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba sasa ikibakiza mechi tatu kabla ya kuhitimisha msimu wa Ligi Kuu 2020/21, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema mipango yake ya kuweza kupata matokeo dhidi Yanga kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho (ASFC) maarufu FA Cup itakayopigwa Julai 25, mwaka huu ipo tayari.

Simba ambayo katika fainali hiyo itavaana na Yanga katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma, Jumamosi iliyopita ilikubali kipigo cha bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Na jana ilishuka katika uwanja huo, kuvaana na wenyeji KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu, wakati ikiwa kileleni mwa msimamo wa ligi na alama zake 73 zilizotokana na kushuka dimbani mara 30, kabla ya mechi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Gomes alisema wamegundua walichokosea katika mechi yao iliyopita dhidi ya Yanga, na tayari ameshalipatia tatizo hilo ufumbuzi huku pia akiamini mechi za ligi zilizobaki zitamsaida kujipanga zaidi kuelekea mchezo huo wa fainali.

Alisema baada ya kupoteza mechi dhidi ya Yanga, walikaa na kujitafakari na kuona wapi walipokosea na sasa hawatakuwa tayari kuona wanapoteza mechi ya fainali.

"Tumeona wapi walipotuzidi wenzetu, nina imani hatuturudia makosa yaliyofanyika katika mechi ya kwanza, tutapambana kuhakikisha tunawafunga katika fainali," alisema Gomes.

Alisema watahitaji kupata matokeo mazuri kwa kila mechi baada ya kuona walipokosea katika mechi iliyopita dhidi ya Yanga, na kwamba wataendelea kufuta makosa hayo kwenye michezo ya ligi na kuhakikisha fainali wanatwaa kombe hilo.

"Mashabiki wetu tunawaomba watuombee hasa kwenye mechi zote ikiwamo FA dhidi ya Yanga. Mechi ni ngumu kwa sababu Yanga wanahitaji kombe hilo kama ilivyo kwetu," alisema Gomes.

Alisema mwanzoni mwa msimu waliwaahidi mashabiki kwamba wanahitaji kutetea ubingwa wa Ligi Kuu na FA, hivyo hana mashaka na ligi kwa sababu wanapambana kutetea taji hilo na baadaye kulipa kisasi kwa Yanga katika FA.

Simba imetinga fainali ya Kombe la FA kwa kuifunga Azam FC bao 1-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Majimaji mjini Songea mwezi uliopita, wakati Yanga ilifika hatua hiyo kwa kupata ushindi kama huo dhidi ya Biashara United kwenye dimba la Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

## Nabi ataja wapya wa kuisuka Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI suala la beki wa kulia wa AS Vita ya DR Congo, Shabani Djuma kujiunga na Yanga likiwa tayari limekamilika, Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Nasreddine Nabi, ameueleza uongozi wa klabu hiyo anahitaji nyota watano ama ikiwapendeza sita ili kukisuka upya kikosi chake kuelekea msimu ujao.

Kocha huyo, ameeleza hatahitaji kukibomoa sana kikosi chake, na wachezaji watakaosajiliwa na timu hiyo ni wale ambao amependekeza kwa uongozi tu na si vinginevyo.

Akizungumza na mwandishi wetu, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema hivi karibuni alifanya mazungumzo na kocha huyo kutaka kujua mapendekezo yake ya kukiimarisha kikosi chake ambapo alimweleza hatafanya mabadiliko makubwa sana kuelekea msimu ujao.

"Kocha alinigusia hatafanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake, na wachezaji atakaowasajili watakuwa watano ama sita tu," alisema Bumbuli.

Kuhusu wachezaji watakaotemwa kupisha usajili huo mpya, Bumbuli alisema: "Ni mapema mno kuwataja, lakini wapo wanaomaliza mikataba yao na wengine ambao watafanya mazungumzo na uongozi kumalizana".

Hata hivyo, kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, wachezaji ambao Nabi amebariki kusajiliwa na timu hiyo mbali na Djuma ni pamoja na David Bryson wa KMC na Dickson Ambuso kutoka Dodoma Jiji FC.

Tangu kutua kwa Nabi, timu hiyo imeonyesha kuwa na muunganiko mzuri huku akiboresha nidhamu kikosini na ikicheza soka la kuvutia tofauti na makocha waliomtangulia katika klabu hiyo msimu huu.

Na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Simba kwenye mchezo wa Ligi Kuu, kumemwongezea Nabi kukubalika ndani ya uongozi wa timu hiyo, wanachama na mashabiki.

Yanga ipo katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 70, tatu nyuma ya Simba iliyopo kileleni huku ikiwa mechi nne nyuma kabla ya mchezo wao wa jana usiku dhidi ya KMC FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >